Jiunge Nasi Katika

# siku za MAOMBI 10

January

03-13 2018

www.TenDaysofPrayer.org

## Ujumbe kutoka Northern Tanzania Union Conference

Kwa waumini wa kanisa la Waadventista wa Sabato katika Northern Tanzania Union Conference na nje ya Union hii; tunawatakia amani na Baraka na furaha, moyo wa kumpenda Mungu na kumtumikia mnapopitia masomo haya ya 'Siku kumi za maombi' kwa mara nyingine tena.

Hatuna budi kumshukuru Mungu kwa jinsi alivyotulinda tangu Januari mwaka jana (2016) tulipokuwa na program hizi. Mungu wetu apewe sifa. Tunawashauri viongozi wa makanisa wahamasishe washiriki kuhudhuria vipindi kila siku, na kwa wakati ili wote wapate kushiriki mibaraka hii. Kadiri invyowezekana, kanisa mahalia lipange muda muafaka utakaowawezesha washiriki wote kuhudhuria.

Ikiwezekana kila Conference wabuni namna ya kufanya wiki hii iwe ni ya pekee na ya kuvutia. Ikiwa kuna visa vyovyote vya namna Mungu alivyojidhihirisha katika siku kumi hizi za maombi, basi visa hivyo vitumwe Union kupitia kwa Makatibu wa Chama cha Wachungaji wa Conference mahalia ili viunganishwe na visa vya sehemu zingine duniani. Bwana awabariki mnapoyapitia masomo haya na kuyaweka katika uzoefu.

Masomo haya yameandaliwa na Idara ya Uchungaji, 'Siku Kumi za Mombi' ya Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato (GC) na kuletwa kwenu na Mchungaji Daniel Ndiegi ambaye ni Katibu wa Chama cha Wachungaji, Northern Tanzania Union Conference. Yametafsiriwa na Moseti Chacha wa kanisa la Waadventista wa Sabato Lemara – Arusha; kisha yakahaririwa na Mchungaji David Maduhu Makoye, Katibu Mkuu wa Northern Tanzania Union Conference.

Ni mimi Mjoli wenu

**Pastor Daniel Ndiegi**
Simu: +255 767 543 904/784 543 904
Baruapepe: dndiegi@yahoo.com

# KUHANI MKUU

**MWONGOZO KWA VIONGOZI**

Karibu katika ziku hizi kumi za maombi mwaka 2018! Mungu amefanya miujiza mingi sana kupitia kwenye program hii ya siku kumi za maombi tangu ilipoanza kidunia mwaka 2006. Roho Mtakatifu ameleta uamsho, uongofu, shauku mpya kwa uinjilisti, na uponyaji kwa mahusiano. Kwa kweli kwenye maombi ndipo mahali uamsho unapozaliwa!

Miongozo imekusudiwa kukusaidia wewe kama kiongozi. Sehemu ya kwanza inashughulika na mada zinazohusiana na siku kumi za maombi za mwaka huu, na sehemu ya pili inajumuisha vielekezo ambavyo vitakusaidia wewe pamoja na kikundi chako cha maombi. Kumbuka kwamba hizi ni nyenzo tu pamoja na dhana. Uwe huru kubadilisha kadiri Roho Mtakatifu atakavyokuongoza.

Katika kipindi cha siku kumi za maombi, yaani Januari 3 hadi 13, 2018 wanachama wa kikundi chako wanatakiwa kukutana kila siku kwa kipindi cha saa moja ya maombi ya pamoja. Siku ile ya kumi na moja, yaani Januari 13 itaangukia siku ya Sabato. Hii itakuwa ni siku ya sherehe ya kushangilia mambo ambayo Mungu ametenda kama majibu kwa maombi yetu ya pamoja. Tunatumaini mawazo na mapendekezo yote yatatusaidia kuzifanya hizi siku kumi za maombi za mwaka huu zilete uzoefu wenye nguvu kwa kikundi hicho kidogo na kanisa kwa ujumla

## Mambo ya kawaida ya maombi katika siku kumi za maombi

***Kwa nini ujifunze kuhusu vazi (joho) la Kuhani Mkuu?*** Kila kitu Mungu anachofanya huwa kina kusudi maalum na sababu ya kuwepo. Hii ni pamoja na hili vazi la Kuhani Mkuu. Katika kitabu cha  Mababu na Manabii (Patriarchs and Prophets) kuna maneno katika ukurasa wa 351 (kiingereza) kuwa "…kila kitu kilichohusiana na mavazi na mwenendo wa makuhani kilitakiwa kuleta mguso wa utakatifu wa Mungu kwa mtazamaji, kuonesha utakatifu wa ibada yake na usafi unaohitajika kwa wale wanaosogelea uwepo Mungu." Na tupitie ishara za mavazi ya kikuhani na kuona kile tunachoweza kujifunza kwa ajili yetu katika karne ya ishirini na moja.

***Ukurasa wa mada ya kila siku:*** Ukurasa wa mada umetayarishwa kwa kila moja ya siku hizi kumi. Ukurasa wa kwanza unapendekeza mpango kwa ajili ya muda wa maombi, dhana mahsusi za maombi pamoja na nyimbo za kuimba pamoja. Ukurasa wa pili una mafungu ya Biblia pamoja na nukuu kutoka kwa maandiko ya Ellen G. White

ambazo zinaongeza nuru katika mada husika. Tunapendekeza kwamba unakili huu ukurasa ili kila mmoja wa kikundi awe na ukurasa mmoja ili kufuatiza wakati wa maombi.

Makanisa ulimwenguni yataunganika katika maombi haya kila siku katika mada ya siku. Jiunge katika maombi kupitia kwenye Maandiko, nukuu na mahitaji ya maombi yalioorodheshwa kila siku. Hata hivo usije ukalazimika kupitia orodha yote ya mahitaji yaliyoorodheshwa ili kuombewa. Mnaweza kugawanyika katika vikundi husika na kila kikundi kuombea baadhi ya mambo katika ile orodha.

Baadhi ya mahitaji katika orodha ya maombi yanamhusu mtu mmoja mmoja na mengine yanalihusu kanisa la Waadventista wa Sabato la ulimwengu. Ni muhimu kuomba pamoja kwa ajili ya mahitaji ya pamoja kama familia ya kanisa, lakini mnaweza kuchagua muda wa kuomba mnaoona unafaa na kuombea mambo ya kawaida hasa ikiwa kuna wageni ambao sio Waadventista wa Sabato. Ombea namna mnavyoweza kupata njia nzuri za kualika wageni na kuwafanya wajisikie sehemu ya kikundi chenu.

***Nukuu za Ellen G. White kuhusu ishara zilizoko katika vazi la Kuhani Mkuu:*** Hapa pameorodheshwa nukuu kutoka katika maandiko ya Ellen G. White na baadhi ya mafungu kila moja ya siku hizi kumi. Nukuu hizi pamoja na mafungu ya Biblia zinaelezea kile kinachowakilishwa na mavazi mbali mbali ambayo Kuhani mkuu alikuwa akivaa. Inapendekezwa kwamba msome nukuu na mafungu haya pamoja katika kikundi chenu. Mnaweza kufanya hivi kabla ya maombi ili kujenga hoja kwa ajili ya mada husika, au kati kati ya kipindi cha maombi.

***Muda unaopendekezwa kwa ajili kila kipengele cha maombi:*** Muda utakaotumia kwa maombi unaweza kutofautiana kila wakati mnapoomba pamoja. Yafuatayo ni mapendekezo yanayoweza kuwa bora:

- Kukaribisha/Utangulizi – dakika 2 hadi 5
- Kusoma mafungu na nukuu za maandiko ya EGW – dakika3
- Kipindi cha ibada ya kusifu katika maombi – dakika 10
- Kipindi cha toba na kuungama pamoja na kudai ushindi dhidi ya dhambi – dakika 3 hadi 5
- Kipindi cha kujitoa na kuingilia kati kwa maombi – dakika 30 hadi 35
- Kipindi cha shukrani katika maombi – dakika 10

***Kumsihi Mungu na kuomba kwa ajili ya watu saba uliowachagua:*** Watie moyo watu wote kumsihi Mungu awaoneshe kila mmoja watu saba ambao atakuwa anawombea katika siku hizo kumi za maombi. Wanaweza kuwa ni wanafamilia, marafiki, wafanyakazi wenza, washiriki wenzako kanisani, n.k. Wahimize waombe kwamba Roho Mtakatifu awaongoze hao watu saba wadumu katika Kriso. Wanakikundi pia wamwombe Mungu awaoneshe jinsi watakavyoombea mahitaji mahususi ili kuwafikia hao watu saba kwa kipindi hiki cha siku kumi za maombi.

***Huduma ya Sabato katika siku hizi kumi za mwaka 2018:*** Maombi na yalenge katika kitu mahsusi mkishiriki shuhuda mbali mbali jinsi Mungu alivyojibu maombi. Jambo hili linaweza kufanyika katika vipindi mbali mbali katika Sabato mbili hizo. Ni vema kuwa wabunifu kuhusisha familia nzima ya kanisa kile ambacho kimekuwa kikitendeka katika mikutano ya maombi siku hizo kumi.

***Sherehe za Sabato ya kuhitimisha:*** Sabato ya mwisho ipangwe mapema, uwe ni wakati wa kujumuika katika furaha ya mambo yote aliyoyatenda Mungu katika kipindi hiki cha maombi ya siku kumi. Tenga muda wa kutosha kwa ajili ya ushuhuda wa maombi yaliyojibiwa, kwa ajili ya mafundisho maalum ya Biblia, mahubiri yaliyotayarishwa vizuri kuhusu umuhimu wa maombi, na nyimbo za sifa kwa Mungu wetu. Kusanyiko liongozwe katika wakati wa maombi ili wale ambao hawakupata nafasi ya kuhudhuria katika siku hizi, washiriki uzoefu wa furaha ya kuomba na wengine. Somo la siku ya kumi na moja lina dhana husika.

***Kufuatilia kipindi hiki cha maombi ya siku kumi mwaka 2018:*** Omba sana ili kujua jinsi Mungu anavyotaka kanisa lako au kikundi chako kiendeleze kile ambacho Amekianzisha katika siku hizi kumi za maombi. Pengine ni vema kuendelea na mikutano ya maombi ya kila wiki, au labda Mungu anataka uanze huduma mpya katika kanisa lako au utoke kuwaendea wengine katika jamii. Uwe muwazi na kufuata kile ambacho Mungu anaelekeza. Utashangaa kadiri unavyotembea naye.

***Ushuhuda:*** Ni vema kushiriki visa vyako jinsi Mungu alivyotenda kupitia kwako katika siku hizi kumi za maombi ya mwaka 2018. Visa vyako vitawatia moyo wengine. Visa hivi vinaweza kutumwa katika Idara ya huduma binafsi kwa baruapepe iitwayo: stories@ministerialassociation.org au kutumwa moja kwa moja kwenye tovuti ya www.tendaysofprayer.org

## Vielekezi vya kuunganika katika maombi

**Kubalianeni:**

Wakati mtu mmoja anapokuwa akimwomba Mungu kwa ajili ya hitaji fulani, hawa wengine nao waendelee kuomba kimya kimya, na hivyo maombi yanaunganika pamoja. Sio kweli kwamba mtu mmoja akiombea haja fulani basi wengine hawa wanabaki wamenyamaza tu, bali wnatakiwa kuunganika katika maombi – huko ndiko kupatana katika maombi. Tunasoma katika Mathayo 18:19 kuwa "Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni." Unapotegemezwa wakati wa maombi katika hitaji fulani basi inatia moyo.

**Kudai Ahadi za Mungu**

Kuna ahadi kadhaa za Mungu zimetayarishwa ili kusaidia watu kudai katika maombi. Wahimize wanakikundi kudai ahadi za Mungu kadiri wanavyoomba. Ni rahisi kujielekeza katika matatizo yetu, lakini tunapodai ahadi za Mungu basi tunaongeza imani yetu na kujikumbusha kwamba hakuna jambo gumu lisilowezekana kwa Mungu. Ahadi zinatusaidia kuondoa fikra zetu katika madhaifu na magumu yanayotukabili, na kuzielekeza kwa Yesu. Kuna ahadi katika Biblia ya kudai tunapokabiliana na changamoto fulani. Wahimize washiriki katika vikundi kutafuta ahadi zaidi na kuziandika ili kuweza kuzidai siku za usoni.

"Tunatakiwa kuwasilisha mahitaji yetu kwenye maombi kwa moyo wa unyenyekevu na kuzieleza kwa uwazi na uhakika huku tukidai ahadi kwa imani hadi kusanyiko zima watambue kwamba tumejifunza kudumu kumsihi Mungu katika maombi. Watatiwa moyo kuanimi kwamba kuna uwepo wa Bwana katika mkutano, kisha watafungua mioyo yao ili kupokea mibaraka yenye utajiri. Imani yao itaongezeka nao watakuwa tayari kusikiliza maagizo yanayotolewa na mzungumzaji kwa masikio yenye utayari." *(Evangelism, uk. 146).*

"Mungu ametayarisha mbingu iliyojaa mibaraka kwa wale ambao watashirikiana naye. Wale wote wanaomtii wanaweza kudai kwa ujasiri kutimizwa kwa ahadi zake. Lakini ni lazima tuoneshe uimara usio yumba yumba wa imani kwa Mungu. Mara nyingi anachelewa kujibu maombi yetu ili kujaribu imani zetu na udhati wa matumaini yetu. Baada ya kuomba sawasawa na Neno lake tunatakiwa kuamini katika ahadi yake na kudumu kusihi kwa dhati, naye hatatukatalia." *(Christ's Object Lesson uk. 145)*

**Kufunga**

Wakaribishe wale mliojiunga katika maombi ya siku kumi za maombi katika aina moja au nyingine ya kufunga, kwa mfano kuepuka kuangalia TV kwa kipindi fulani, muziki, intaneti, mitandao ya kijamii, vitafunwa vitamu vitamu, au vyakula aina ile inayokuwa ngumu kumeng'enywa. Tumia wakati wa ziada kujifunza Biblia, zungumza na Mungu na kumwomba awasaidie katika kikundi chenu na kusanyiko lote kwa ujumla ili kudumu kwa utimilifu ndani ya Kristo. Kwa kutumia lishe ya kawaida iliyo rahisi, hawa wanakikundi wataruhusu fikra zao kupata uweo wa kusikia na kupokea sauti ya Roho mtakatifu.

**Roho Mtakatifu**

Ni vema kuwa na uhakika kwamba tumemwomba Roho Mtakatifu atuoneshe jinsi ya kuomba na mambo ya kuombea katika maisha kwa hali fulani mahususi. Biblia inatuambia kwamba hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.

"Hatuna budi kuomba sio tu kwa jina la Yesu Kriso, bali pia kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Kufanya hivi kunaelezea maana ya kusema Roho Mtakatifu hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. (Warumi 8:26). Mungu anafurahia kujibu maombi kama hayo. Tunapopumua maombi kwa udhati wa pekee kwa jina la Kristo, panakuwa na ahadi kutoka kwa Mungu kwamba anaenda kujibu hayo maombi kama ilivyoandikwa, *"Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu"* (Waefeso 3:20) *(Christ's Object Lessons, uk. 147)*

**Kuwa Pamoja Kimwili**

Mnapoanza kuingia katika maombi ya kuunganika, karibisha kila mmoja aje kushiriki. Watu wanapounganika pamoja katika mduara ulio imara, inasaidia kukuza roho ya umoja ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya maombi ya muunganiko. Ikiwa watu watatawanyika katika chumba, itakuwa ni vigumu kusikilizana wakati wa maombi.

**Kutunza taarifa ya maombi**

Zoezi la kutunza taarifa ya maombi katika siku hizi kumi litakuwa ni namna iliyo nzuri ya kushiriki kuzamisha zile mada za kila siku katika fikra za wanakikundi na kusaidia katika kufanya maamuzi thabiti kwa Mungu, na kutambua mibaraka yake kwao.

Kuorodhesha maombi yaliyofanywa na kutunza taarifa ya maombi yaliyojibiwa ni namna iliyothibitishwa ya kutia moyo.

Kuna namna kadhaa mabazo unaweza kujumuisha hii orodha katika maombi haya ya siku kumi. Unaweza kutenga muda wakati wa maombi ili wanakikundi waorodheshe maombi yao na jinsi Mungu alivyowajibu. Au unaweza kutunza yale mambo mnayoombea na ikiwa yamejibiwa basi kuyaweka kwenye bango kubwa au kuyarusha kwenye mtandao. Unaweza kufanya hivi kwa kuchora msitari kati kati ya karatasi, kisha ukawa na maombi upande mmoja na majibu upande mwingine. Inafurahisha na kujenga imani unapoona jinsi Mungu anavyojibu maombi yaliyoorodheshwa.

**Kicho**

Himiza na kukuza hali ya kucho kwa wanakikundi. Tunakabili chumba chenye kiti cha enzi cha Mfalme wa ulimwengu. Hebu tusichukulie kipindi hiki cha maombi kwa uzembe katika mkao wetu au mwenendo. Sio lazima kwamba kila mtu apige magoti muda wote, watu na wauone muda huo wa maombi kama muda maalum wa kufurahisha, hivyo wahimize watu wapige magoti au kukaa au kusimama kadiri Mungu atakavyowaongoza na kulingana na anavyoona nafuu kwake.

**Maombi kwa Sentenso**

Maombi na yawe mafupi, na yaelekezwe moja kwa moja kwenye hitaji. Kufanya hivi kutawapatia wengine pia fursa ya kuomba. Jaribu kufupisha ombi lako kwa sentenso chache, kila mmoja anaweza kuomba mara kadhaa. Maombi mafupi yatafanya kipindi cha maombi kuwa cha kufurahisha na sio cha kuchosha huku mkimruhusu Roho Mtakatifu kugusa vikundi na kuwaongoza akiwaonesha namna ya kuomba. Sio lazima kuanza na kumaliza kwa maneno “Mungu wetu mpendwa” na “Amina” kwa sababu ni maombi endelevu kwa mawasiliano na Mungu

**Ukimya**

Wewe kama kiongozi sio vema utawale kipindi cha maombi. Lengo kubwa ni kuwawezesha wengine kuomba. Kipindi cha ukimya kina thamani kubwa ajabu, kwani kinampa Mungu muda wa kuzungumza na mioyo yetu. Ruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi kwa kumpa kila mmoja muda wa kutosha wa kuomba.

**Kuimba**

Nyimbo za hapa na pale kutoka kwa vikundi zikichanganywa kwenye maombi, zinaongezea uzuri wa mkutano wa maombi. Nyimbo zinazofaa ziorodheshwe kabla ya kipindi, sio lazima ziimbwe zote ila kwa wakati muafaka kama itakavyohitajika. Kuimba pia ni njia nzuri ya kuhama kutoka kwenye kipindi kimoja kwenda kwenye kipindi kingine.

**Kukusanya Mahitaji ya Kuombea**

Usiulizie mahitaji ya kuombea kutoka kwenye kikundi. Badala yake, waambie watu wataje mahitaji yao katika maombi na kuwahimiza wengine kujiunga wakikubaliana nayo kwa kuungana katika maombi kimya kimya. Sababu kubwa ni kwamba, muda unaweza usitoshe kwa kuombea mahitaji ya mtu mmoja mmoja. Ukitaka kuzungumza kuhusu mahitaji ya kila mmoja unaweza kutumia muda wote wa maombi. Shetani anafurahi anapoona tunatumia muda wa maombi kuzungumza kuhusu matatizo yetu badala ya kuombea hayo matatizo. Wanakikundi wanaweza kuanza kushauriana na kupendekeza ufumbuzi. Uwezo unatoka kwa Mungu. Kadiri tunavyoongeza maombi ndivyo anavyoachia uwezo wake.

**Muda wako wa kila siku**

Ni muhimu wewe kama kiongozi kuhakikisha unatumia muda wako mwingi katika miguu ya Yesu, ukizungumza naye na kusoma Neno lake. Ikiwa utafanya kumfahamu Mungu kuwa kipaumbele chako katika maisha, utafunguliwa uzoefu ulio mzuri wa ajabu. "Nguvu ya ajabu inayoweza kutingisha dunia hutoka katika sehemu yako ya siri ya maombi na kuleta matengenezo makuu. Pale mahali pa siri akiwa katika utulivu, mtumishi wa Bwana anaweka miguu yake katika mwamba wa ahadi za Mungu. *(The Great Controversy, uk. 210)*

## UTANGULIZI

Karibu katika siku kumi za maombi mwaka 2018! Tunamshukuru Mungu kwamba tunaweza tena kuuanza mwaka huu kwa maombi. Mungu amefanya miujiza miaka iliyopita kwa kadiri tulivyomwomba kwa kufunga. Roho Mtakatifu ameleta uamsho, uongofu na shauku mpya ya uinjilisti na uponyaji katika mahusiano yetu. Kusema kweli katika maombi ndipo mahali ambapo uamsho huzaliwa.

Tunaamini kwamba maisha yako na maisha ya wale unaowaombea yatabadilishwa kadiri unavyojiunga na washiriki wengine kanisani kwako katika kuomba kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ambaye Baba yetu ameahidi kuwapa wale wamwombao.

**Mada yetu ya Maombi: Kuhani Wetu Mkuu**

Katika siku hizi kumi za maombi tutapitia na kuona kwamba mavazi ya Kuhani Mkuu wa Agano la Kale yanatupa fundisho gani.

Tunasoma katika Tumaini la Vizazi vyote kwamba, "Kila vazi alilovaa kuhani lilitakiwa kuwa kamili bila waa lolote. Kwa mavazi mazuri hayo yaliyokuwa rasmi, tabia ya Yesu Kristo iliwakilishwa. Kile kilichoonekana ni ukamilifu wa mavazi na mwonekano, kwa maneno na kwa roho, ili aweze kukubalika mbele za Mungu. Yeye ni Mtakatifu, na utukufu wake na ukamilifu wake ni lazima uwakilishwe katika huduma ya hapa duniani. Ni ukamilifu pekee ndio ungewakilisha ule utakatifu wa huduma ya mbinguni. (*Desire of Ages* uk. 705)

Kila vazi alilovaa kuhani na kila huduma aliyofanya ilikusudiwa kuacha mguso wa namna fulani kwa watu. "Kila kitu kilichohusishwa na vazi na mwenendo wa kuhani kilikusudiwa kuacha mguso kwa watazamaji wapate kutambua utakatifu wa Mungu, udhati unaohitajika katika kumwabudu, na usafi unaohitajika kwa wale wanaosogelea uwepo wake." (*Partriachs and Prophets*, uk. 351). Katika siku hizi kumi za maombi, tutagundua baadhi ya masomo ya kiroho yanayowakilishwa na mavazi ya kuhani.

**Mwongozo unaopendekezwa wakati wa maombi**

- Jitahidi kufanya maombi yawe mafupi – sentensi moja a mbili kuhusu mada moja. Kisha waachie wengine. Unaweza kuomba mara nyingi kadiri unavyojisikia, kwa namna ile ile unayozungumza na rafiki.
- Msiogope kuwa kimya kwani kwa kufanya hivyo mtakuwa mnapata muda wa kumsikiliza Roho Mtakatifu.

- Imbeni nyimbo pamoja kadiri Roho Mtakatifu atakavyowaongoza, huo pia ni mbaraka mkubwa. Wala hamhitaji kinanda ili kuwaongoza, imbeni tu bila kinanda, inapendeza
- Badala ya kutumia muda mwingi mkijadili matatizo na mahitaji ya kila mmoja, ni vema kuyaomba tu. Wengine pia wanaweza kuomba na kutaja mahitaji yao katika maombi kila mmoja huku wakidai ahadi zinazoambatana na mahitaji hayo.

**Kudai Ahadi**

Mungu ametupatia ahadi nyingi katika Neno lake. Ni faida kwetu kudai ahadi hizo katika maombi. Maagizo yote ya Mungu na mashauri yake pia ni ahadi, kwani hawezi kudai jambo fulani kutoka kwetu ambalo hatuwezi kufanya kwa uweza wake.

Tunapoomba, ni rahisi kujielekeza katika mahitaji yetu, changamoto zetu au labda manung'uniko kuhusu hali fulani inayoweza kuwa imetokea. Hili silo kusudi la maombi, kusudi kubwa la maombi ni kuimarisha imani yetu. Ndiyo maana tunahimizwa kudai ahadi ambazo Mungu ametupatia katika maombi yetu. Ahadi zitakusaidia kuhamisha macho yako kutoka katika mahitaji yako na changamoto zako na kuyaelekeza kwa Yesu Kristo. Ni kwa kumwangalia yeye ndipo tunapobadilishwa na kuchukua sura yake.

Kila ahadi katika Neno la Mungu ni kwa ajili yetu. Ni katika maombi pekee ndipo tunapoweza kuwasilisha haja zetu, kwa kuonesha kwenye Neno la Yehova, na kwa imani kudai hizo ahadi. Neno lake linatupatia uhakika kwamba ukiomba kwa imani, utapokea mibaraka yote ya kiroho. Endelea kuomba nawe utapata zaidi ya kile ulichoomba. (*Heavenly Places,* uk. 71).

Utadaije hizo ahadi za Mungu? Kwa mfano, unapoomba kwa ajili ya amani, unaweza kudai Yohana 14:27 na kusema, "Bwana umetuambia katika Maandiko yako kwamba 'Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.' Ninakuomba unipatie amani uliyoahidi kutuachia." Kisha umshukuru Bwana kwamba atakupatia hiyo amani hata kama haujisikii kuwa na amani wakati huo.

**Kuombea watu saba**

Tunawahimiza kuomba kwa siku hizo kumi kwa namna maalum kila mmoja akiombea watu saba ambao angependa kuona wakipitia uzoefu wa "kuwa na uzima kisha kuwa nao tele." Hao wanaweza kuwa ni jamaa wa karibu, marafiki, wafanyakazi wenza, majirani, au watu mliozoeana nao. Tenga muda wa kutosha wa kuzungumza na Mungu ili akuoneshe ni nani angependa umwombee. Mwombe Mungu akupatie namna ya kuelewa mizigo waliyo nayo ili upata kuiwakilisha kwake.

## USIKU WA MAOMBI

*Kwa nini kuwa na usiku wa maombi?*

Hakuna kitu kitakatifu kama kukesha ukiomba usiku kucha au sehemu ya usiku. Hata hivyo, usiku unaweza kuwa ndio muda pekee ambao watu hawakushikika kwa shughuli za kila siku, au hawako katika hali ya haraka haraka. Tunaamini kwamba kusudi lako sio kukesha usiku kucha bali ni kupata muda wa kutosha wa kuzungumza na Mungu, kumweleza haja zako zote ambazo anataka uziombee.

Pendekezo ni kwamba watu wachache waongoze maombi usiku huo. Ni vema kuwa na vipindi vya mapumziko. Kama kiongozi unaweza kukadiria muda muafaka wa kupumzika kulingana na unaovyoona hali halisi, hasa unapotaka kuhama kutoka katika hatua moja kwenda katika hatua nyingine ya maombi. Tunapendekeza kwamba pawepo na pumziko la angalau dakika kumi kila baada ya kipindi cha dakika tisini. Unaweza kuunganisha usomaji wa Biblia katika ule muda wa maombi. Sio lazima ufanye yote yaliyopendekezwa, itategemea kile ambacho unaona ni bora kwa kikundi chako. Usione shaka kubadilisha pale unapoona panastahili.

Mapendekezo ya maombi ya usiku ni kama ifuatavyo

- **Anza na kipindi cha kusifu:** Msifu Mungu katika maombi yako na pia kwa nyimbo.
- **Ingia katika kipindi cha toba na maungamo:** Uwe na uhakika kwamba hakuna kitu kinachozuia Mungu asikusikie. Wapatie watu nafasi ya faragha ya kuungama kila mmoja binafsi, kisha pawe na muda wa maungamo ya pamoja. Wahimize watu kuungama dhambi za siri wakiwa faragha na kuungama zile dhambi zisizo za siri hadharani. Katika Danieli 9:1-19 tuasoma kuhusu Danieli ambaye alikuwa akiungama hadharani dhambi za watu wa Mungu. Wahimize watu waungame dhambi za hadhara za kanisa.
- **Ombea mahitaji ya wale waliopo katika mkutano wa maombi:** Watu wengi wanatamani wangepata muda wa kuomba, au pengine unamfahamu mmoja ambaye amekata tamaa na anahitaji maombi. Tengeneza mduara na uweke kiti katikati, kisha wale ambao wana haja binafsi ambazo wangependa ziombewe wapite kati na kukaa mmoja baada ya mwingine aombewe. Kisha kusanyika wakimzunguka Yule anayeombewa na kuchagua watu wawili kumwombea kwa sauti kwa mahitaji yake huku wakidai ahadi za Mungu katika maombi hayo. Utashangaa wingi wa watu wanaoteseka na kuhitaji maombi ya jinsi hii.

- **Gawanya kikundi chako na kutengeneza viwili:** Waelekeze wanakikundi wenye jinsia ya kike kwenye chumba kimoja na wale wa jinsia ya kiume katika chumba kingine. Chagua kiongozi katika kila chumba. Wakati mwingine kuna haja za faragha kwa jinsia maalum ambazo haziwezi kushirikishwa jinsia nyingine
- **Baada ya kukutana pamoja:** Ombea orodha ya mahitaji kulingana na orodha iliyo chini hapa. Mahitaji haya yamekusanywa kutoka sehemu zote za kanisa duniani. Ni vema ukagawanya watu katika vikundi vidogo vidogo na kuwagawia mahitaji hayo.
- **Ombea watu saba:** Wale ambao umeorodhesha ili kuwaombea kwa siku hizi kumi.
- **Chagua fungu la Biblia litakalotumika kuombea hitaji fulani.**
- **Funga muda wa maombi kwa kuanza kipindi kingine cha shukrani.**

Mahitaji ya kuombea

1. Ee Bwana, tunaomba uwezeshe kanisa letu lipate kumwinua Yesu Kristo aliyesulubiwa na anayekuja tena. Tupatie kuelewa uzito wa roho zinazopotea.
2. Tunaomba ubariki shughuli za kiinjilisti zitakazofanyika kuwafikia watu duniani kote mwaka ujao. Tunaomba hasa kwa ajili ya jitihada za uinjilisti wa kuwashirikisha washiriki wote (TMI) kule Japan, Zambia na Philippines
3. Tunaomba kwa ajili ya uamsho wa kiroho kati ya vijana wa ki-Adventista walio katika mshule na vyuo visivyo vya kanisa letu duniani kote. Tunaomba uwafanye kuwa mabalozi wema wa Kristo huko waliko.
4. Bwana tunaomba ubariki kazi ya Umisionari wa ki-Adventista. Wapatie watendakazi wetu hekima kadiri wanavyoratibu zoezi la kuanzisha makanisa duniani kote huku wakitafuta fedha za kupeleka waanzilishi wa utume ulimwenguni katika maeneo ambayo hayajafikiwa bado.
5. Wabariki washiriki wa kanisa walio waaminifu wanaotegemeza kazi yako kwa kuwepo wenyewe au kwa mali na vitendea kazi wanavyotoa ikiwa ni vidogo au vikubwa. Tuguse kwa namna ya pekee kila mmoja wetu ili tupate kutoa kwa hiari na kupokea mibaraka inayoambatana na uaminifu katika uwakili.
6. Bariki jitihada za huduma ya uchaplensia kadiri wanavyowezesha wachaplensia na wengine wote wanaojitolea kuhudumia walio magerezani, mahospitalini, majeshini na maeneo mengine. Wafanye walete matumaini na uponyaji wa kiroho kwa watoto wako waliosahauliwa.

7. Bariki kazi inayofanywa na shirika la misaada la ADRA kadiri wanavyokabiliana na mahitaji mbali mbali ya masikini na wale waliosahauliwa.
8. Bwana tunakuomba uimarishe imani yetu na kutuongoza katika kutenga muda wa kutosha kujifunza Biblia na kuomba. Hebu tutembee na wewe kila siku kama vile Henoko alivyotembea na wewe.
9. Tunaomba ubadilishe mioyo yetu ielekee katika mambo ya umilele badala ya mambo ya dunia hii yanayovuta katika maovu. Tulinde kutoka katika mivuto ya kidunia ambayo inatishia uzoefu wetu wa kiroho wa kila siku
10. Baba, mapenzi yako na yatimizwe katika maisha yetu na katika kanisa letu badala ya mapenzi yetu. Tunyenyekeze na kutufanya tunaoweza kufundishika tukiwa tayari kukumbatia mipango yako.
11. Tunaomba utuongoze kila mmoja wetu katika kujikana nafsi na kuishi kwa uwezo wa Yesu Kristo. Tunaomba kwamba uwaongoze vijana kutoa maisha yao katika kazi yako.
12. Bwana, inua utukufu, nyenyekeza viongozi wa kanisa lako ili wadhihirishe tabia ya Kikristo katika maneno yao na matendo yao. Tuoneshe jinsi tutakavyowategemeza viongozi wetu kwa maombi, kuwatia moyo na kuwa tayari kutumika.
13. Tunaomba kanisa lako litangaze ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14 kwa uaminifu na kwa ukamilifu wake. Tupatie hekima ya kuifanya haki ya Kristo iwe ndiyo kiini cha ujumbe huu.
14. Bariki jitihada zetu kadiri tunavyopanga "Vituo vya Mvuto" katika miji mikubwa duniani. Tupatie uwezo wa kuona na kupambanua sehemu zenye uhitaji katika kila mji. Tupatie ubunifu wa kuweza kukabiliana na mahitaji ya sehemu husika. Tuoneshe jinsi ya kuwaongoza wengine katika Neno lako kwa upendo.
15. Bwana tunaomba utupe uamsho na matengenezo katika maisha yetu wenyewe, katika familia zetu, kanisani kwetu, na katika jamii yetu kwa ujumla. Tunakuomba uanze kwa kubadilisha mioyo yetu ili kwamba neema iweze kumiminika kupitia kwetu kwenda kwa wengine.
16. Bwana tunaomba uguse Waadventista wa Sabato kote ulimwenguni wapate kuomba kwa namna ambayo hawajawahi kuomba. Tuwezeshe kuomba na kusihi kwa pamoja kwa ajili ya kumwagwa kwa mvua ya masika ya Roho Mtakatifu. Tunaomba utimize ahadi yako iliyopo katika Yoeli 2, Hosea 6 na Matendo 2.

17. Tunaomba Bwana uwalinde vijana kutoka katika majaribu ya dunia hii. Geuza macho yao yamwelekee Yesu Kristo na uwasaidie kutoa wakfu muda wa maombi na kujifunza Biblia kila siku.
18. Baba, tafadhali utufundisha jinsi ya kushiriki na wengine mkate wa uzima. Tunapokuwa dhaifu, tutegemeze. Tunapoingiwa na hofu, tupatie ujasiri wako.
19. Tunaomba utupatie mtazamo mpya tunaposoma na kujifunza kitabu cha Danieli na ufunuo, na vitabu vingine vya unabi. Tafadhali uwapatie washiriki wa kanisa letu tumaini imara kwa mambo yajayo na uelewa dhahiri wa pambano kuu kati ya Kristo na Shetani.
20. Bwana tufundishe namna ya kujifunza Neno lako kila siku. Uwaguse washiriki wengi zaidi katika mpango wa "Uamini Unabii Wake" kwa kusoma Biblia na vitabu vya Roho ya Unabii kwa pamoja kama kanisa.
21. Tusaidie kila mmoja wetu kuthamini na kutafuta hekima yenye uvuvio iliyotolewa kwa ajili ya kanisa katika maandiko ya Roho ya Unabii. Hebu mashauri haya na yatuongoze kwa undani kwenye ulimwengu wako, ambao ni Biblia.
22. Bwana tuoneshe jinsi ya kutoa maisha yetu kwako kwa ukamilifu. Tufanye wamoja na Kristo. Tuunganishe katika kutangaza kilio kikuu cha mwisho kwa ulimwengu
23. Bwana umelibariki kanisa letu kwa uelewa mkubwa wa ukweli wa Biblia, tunakuomba utuwezeshe kuushiriki ukweli huu kwa unyenyekevu na ulimwengu unaotuzunguka.
24. Baba, tafadhali bariki jitihada za vikundi vidogo na makanisa yaliyo kwenye nyumba za watu kote ulimwenguni. Tunakuomba uinue washiriki waaminifu watakaoshuhudia kumhusu Yesu Kristo na tabia yake nzuri kwa majirani wao.
25. Bwana tufundishe jinsi ya kutangaza misingi ya imani ya kanisa letu kwa uwazi na ubunifu utokao katika umahiri wa Biblia. Hebu upendo wa Kristo uwe ndio kiini cha mambo yote tunayoamini.
26. Hebu familia zetu na zidhihirishe upendo wako katika jamii yetu. Tunakuomba ulete uelewano majumbani, ponya mahusiano yaliyovunjika, walinde wasio na uwezo kutoka katika kunyanyaswa, na udhihirishe uwezo wako utakasao katika hali isiyo na matumaini.
27. Bwana, tunaombea maelfu ya waanzilishi wa utume ulimwenguni ambao wanaanzisha makanisa katika maeneo yasiyofikiwa. Wengi wao wanafanya kazi peke yao katika mazingira magumu kwa hiyo tunaomba kwa ajili ya usalama wao, uwahekimishe na kuwafanikisha.

28. Bariki jitihada za Mtandao wa Wataalam wa Kiadventista. Wapatie fursa za kimbingu ili wafanye utume kwa wanataaluma na wasomi katika maeneo ya dunia yaliyopo mijini.
29. Tunakuomba uwapatie ulinzi wa pekee washiriki wa kanisa wanaokabiliana na manyanyaso au vitisho kwa usalama wao kwa sababu tu ya imani yao. Tuaomba uwapatie hekima na ujasiri. Utuguse tupate kuishi kama mashahidi katika ulimwengu ambao haukufahamu.
30. Tunaomba kila mshiriki wa kanisa la Waadventista wa Sabato duniani apate maono ya ushirikishwaji wa washiriki wote (TMI). Tuwezeshe kila mmoja wetu kuwa hai katika ushuhudiaji binafsi, na vikundi vidogo vidogo vinavyoifikia jamii au umma kwa uinjilisti.
31. Tafadhali tuma Roho wako Mtakatifu atayarishe mioyo ya wasikilizaji wa Radio ya Waadventista wa Sabato ulimwenguni, hasa maeneo ya dunia yaliyoko mijini. Wajalie washiriki kuwa waaminifu kufuatilia na kuwafanya wale wanaokutafuta kuwa wanafunzi wako.
32. Wabariki washirika wa kanisa letu kama shirika na kutegemeza huduma mbali mbali katika kazi yako kuu ya kuwafikia watu kwa uinjilisti. Wajalie watumishi wako kufanya kazi pamoja wakipendana kila mmoja na mwenzake huku wakikupenda wewe.
33. Bwana tafadhali tuoneshe jinsi ya kupeleka vijuzuu vilivyojawa na kweli (vile vilivyochapishwa pamoja na kwenye mtandao) katika jamii inayotuzunguka. Inua wainjilisti wengi wa vitabu, wanafunzi wanaojitolea, waandishi, wataalam wa mitandao, na watu wenye fedha watakaotegemeza uenezaji wa Neno na tumaini la maisha ya milele.
34. Tunaomba uwezeshe kusambazwa kwa miongozo ya Biblia, majarida, na vitabu kama "Jipatie Amani Moyoni". Hebu haya machapisho na yapande mbegu ya ukweli ndani ya mioyo ya watu na kuwaongoza kujifunza Neno la Mungu.
35. Tunaomba uwawezeshe washiriki, wachungaji, na viongozi wengine duniani kote kujilisha katika Neno lako kila siku. Sisi pia utuwezeshe kukutafuta kila siku katika maombi binafsi. Utukumbushe kwamba hatuwezi kufanya jambo lolote bila wewe.
36. Tunakuomba Bwana utufanye kuwa tayari kukufuata katika nyanja za maisha yetu yote. Tunapotaka kupiga hatua inayofuata ya utii, utuoneshe ni ipi. Jaza maisha yetu kwa uwezo wako.

37. Tunakuomba uhuishe mahudhurio ya Shule yetu ya Sabato duniani kote. Waongoze washiriki wote pamoja na wageni kupitia uzoefu wa uhusiano utokanao na badiliko la maisha, utume, kujifunza Biblia na kutoka na kuwaendea watu kama kanisa.
38. Tunakuomba uimarishe huduma ya kutoka na kuifikia jamii kwa kila kanisa mahalia. Huduma kama vile huduma za wanawake, Pathfinder, Adventurers, na huduma ya Waadventista kwa jamii. Tuoneshe jinsi ya kuwa "mkono wako na miguu yako" kwa wengine.
39. Bwana, tunakuomba uwezeshe uwepo wa uamsho ule wa kale katika kanisa lako katika siku hizi za mwisho. Tuwezeshe kusimamia ukweli hata kama mbingu zingeanguka.
40. Wabariki mashuhuda wa huduma ya mitandao ya Waadventista wa Sabato pamoja na mitandao ya kijamii. Wasaidie kuhakikisha wanakuwa bora kadiri tunavyowakaribia watu wa karne ya ishirini na moja tukiwa na injili ya milele.
41. Bwana tupatie hisia za kustaajabu na kushukuru kadiri tunavyotafakari ulimwengu uliouumba. Tunaomba utuwezeshe kuuheshimu ukweli wa Biblia unaohusu uumbaji na kufundisha vijana wadogo kutambua uwezo wako na upendo wako katika uumbaji wako wa asili.
42. Bwana, tufundishe kufuata mfano na kielelezo cha Yesu Kristo ambaye hakuwa na ubinafsi kabisa kwa kukabiliana kila siku na mahitaji ya watu walio karibu na sisi. Tuwezeshe kutumika kama wamisionari matabibu, wanaojitolea katika jamii, na rafiki wa wenye shida.
43. Tuoneshe jinsi ya kushughulikia mahitaji ya wakimbizi ya kimwili na ya kiroho. Hebu kanisa letu lifahamike kwa upendo uliopo kwa watu wote bila kujali ni kina nani, au wanatoka wapi.
44. Tunaomba kwa namna ya pekee kwa ajili ya wakimbizi futoka katika nchi ambazo zimefungiwa injili isitangazwe. Kadiri tunavyowatimizia mahitaji yao basi waongozwe kukufahamu wewe zaidi. Tunaomba ufungue milango kwamba waweze kurudi nchini kwao nakushiriki na wengine upendo wa Mungu
45. Baba, tafadhali tupatie hisia za juu za kuelewa umuhimu wa kazi tunayofanya kwa ajili yako. Tuwezeshe kuishi tukiwa na tumaini kila siku kwamba Yesu anakuja hivi karibuni kufanya mambo yote kuwa mapya.
46. Bwana tunakuoba ubariki kazi ya Waadventista wa Sabato wanaofundisha katika ngazi zote duniani kote. Waimarishe waalimu mashuleni, wazazi,

viongozi wa vijana, na waalimu wa Shule ya Sabato kadiri wanavyotayarisha kizazi hiki cha vijana kwa ajili ya kukutumikia.

47. Tunakuomba uinue wamisionari ambao ni matabibu ili waanzishe makanisa kati ya makundi 830 ya watu kwenye nchi 11 za Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati.
48. Tunakuomba ubariki kazi ya Huduma ya wahitaji maalum. Tupatie moyo wa huruma kadiri tunavyotafuta kutatua mahitaji ya wale wenye shida kama, viziwi, vipofu, na wengine ambao wana mapungufu mbali mbali ya kimaumbile.
49. Tunakuomba uinue vijana waanzishe makanisa kwa ajili ya makundi 750 ya watu ndani ya nchi 13 za Divisheni ya Euro-Asia.
50. Tunakuomba uinue watendakazi mijini ili waanzishe makanisa kwa ajili ya makundi 806 ya watu ndani ya nchi 20 za divisheni ya Inter-European
51. Tunakuomba uinue jeshi la watendakazi watakaoanzisha makanisa kwa ajili ya vikundi 948 vya watu ndani ya nchi 38 za Divisheni ya Inter-America
52. Tunakuomba uinue wafia dini ambao wapo tayari kufanya kazi ndani ya makundi 746 ya watu katika nchi 20 za Union ya Middle East North Africa.
53. Tunawaombea viongozi wa shughuli za kibiashara za Kiadventista ili washuhudie upendo wa Kristo kati ya makundi 691 ya watu katika nchi 8 za Divisheni ya Amerika Kaskazini
54. Tunakuomba ufungue fursa za kufundisha wamisionari wa kuanzisha makanisa katika makundi 676 ya watu katika nchi 9 za Divisheni ya Amerika Kusini.
55. Tunakuomba kwa ajili ya makundi 541 ya watu ndani ya nchi 18 za Divisheni ya Southern Africa-Indian ovean
56. Tunaomba Mungu atayarishe wanaojitolea ili wakatumike kwa makundi 70 ya watu ndani ya Field ya Israeli.
57. Tunamwomba Mungu awaite waalimu na waelimishaji waliostaafu ili watumike kuhudumia makundi 2,566 ya watu ndani ya nchi 14 za Divisheni ya Southern Asia-Pacific.
58. Tunakuomba uinue mashujaa wa maombi waingilie kati kwa ajili ya makundi 2,568 ya watu ndani ya nchi 4 za Divisheni ya Kusini mwa Asia.
59. Tunakuomba uinue mashujaa wa maombi ili waingile kati kwa ajili ya makundi 893 ya watu ndani ya nchi 25 za Divisheni ya Trans-Europe
60. Tunakuomba uinue wauguzi na madaktari ili waanzishe makanisa kati ya makundi 1,978 ya watu wa nchi 22 za Divisheni ya West-Central Africa

61. Tunakuomba uinue vijana watakaokuwa mitume kati ya makundi 1,459 ya watu ndani ya nchi 20 za Divisheni ya Kusini mwa Pacific
62. Tunakuomba utupe hekima ya kuzifikia tamaduni za kidunia ambazo hazina shauku ya dini ya aina yoyote. Hebu Roho Mtakatifu na avunje kuta ambazo zinaizunguka mioyo hiyo.
63. Bwana tuoneshe jinsi ya kushiriki Injili na makundi ya Waislamu. Tunaomba kwamba uwape usikivu utakaowafanya waitikie na kukubali neema utoayo bure.
64. Tunaombea makundi ya watu katika Asia pamoja na Wabudha, Wahindu na wengine. Wengi wameshasikia jina la Yesu, tunaomba utupatie hekima ya kuelewa mahitaji yao na kuifikia mioyo yao
65. Tubariki kadiri tunavyowafikia watu waliofungwa na roho ya ibada ya sanamu na wale wengine wote wenye imani za mizimu. Tusaidie kuelewa matazamo mpana wa kidunia na kuwasogeza karibu na Mwokozi.
66. Bwana tufanikishe kulifikia lile dirisha la 10/40, ambalo ni sehemu ya dunia yenye mguso mdogo sana wa mvuto wa Kikristo. Fungua mioyo ya watu wapokee habari njema ya Yesu. Hebu wezesha watu wauone upendo wako katika maisha yetu.

SIKU YA KWANZA:

## MAFUTA YA UPAKO

**Fungu elekezi:** Zaburi 133:1, 2

“Tazama, jinsi ilivyo vema, na kupendeza, Ndugu wakae pamoja, kwa umoja. Ni kama mafuta mazuri kichwani, Yashukayo ndevuni, ndevu za Haruni, Yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake.”

**MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA**

**Kusifu**

- Bwana tunakusifu kwa ajili ya ahadi ya Roho wako Mtakatifu
- Tunakusifu kwamba Roho yako inatolewa kwa wale wanaoomba
- Ahsante kwamba Roho Mtakatifu anaweza kuleta umoja kati ya washiriki kanisani.

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama katika mioyo yetu. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhambi zetu.
- Utusamehe tunaposhindwa kufungua mioyo yetu kikamilifu kwa utendaji wa Roho Mtakatifu
- Utusamehe kwa kuwa hatuishi na kutenda kazi kwa umoja na wengine kila siku.

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Baba, tusaidie kuona hitaji letu la Roho Mtakatifu. Tunamwomba Roho wako Mtakatifu atuongoze katika kweli yote kulingana na Yohana 16:13
- Tupatie mioyo iliyonyenyekea ambayo itatafuta kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao kulingana na Waebrania 12:14
- Tafadhali tupatie Roho Mtakatifu atufundishe na kutukumbusha yote uliyotuambia kulingana na Yohana 14:26
- Bwana, tunaomba Roho wako Mtakatifu atusaidie udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, atufundishe namna ya kuomba (Warumi 8:26)
- Bwana, tunaomba kanisa lako limwinue Kristo, yeye aliyesulubiwa na ambaye atakuja tena. Tupatie hisia za mzigo wa roho zinazopotea

- Tafadhali bariki shughuli za kiinjilisti zinazofanyika ili kuwafikia watu ambao hawajakujua katika mwaka huu ulimwenguni pote. Tunaomba hasa kwa ajili ya jitihada za uinjilisti wa kushirikisha washiriki wote (TMI) kule Japan, Zambia na Philippines
- Tunaomba kwa ajili ya uamsho wa kiroho kati ya vijana wa ki-Adventista walio katika mshule na vyuo visivyo vya kanisa letu duniani kote. Tunaomba uwafanye kuwa mabalozi wema wa Kristo huko waliko.
- Bwana tunaomba bariki kazi ya Umisionari wa ki-Adventista. Wapatie watendakazi wetu hekima kadiri wanavyoratibu zoezi la kupanda makanisa duniani kote huku wakitafuta fedha za kupeleka waanzilishi wa utume ulimwenguni katika maeneo ambayo hayajafikiwa bado.
- Wabariki washiriki wa kanisa walio waaminifu wanaotegemeza kazi yako kwa kuwepo wenyewe au kwa mali na vitendea kazi wanavyotoa ikiwa ni vidogo au vikubwa. Tuguse kwa namna ya pekee kila mmoja wetu ili tupate kutoa kwa hiari na kupokea mibaraka inayoambatana na uaminifu katika uwakili.
- Bariki jitihada za huduma ya uchaplensia kadiri wanavyowezesha wachaplensia na wengine wote wanaojitolea kuhudumia walio magerezani, mahospitalini, majeshini na maeneo mengine. Wafanye walete matumaini na uponyaji wa kiroho kwa watoto wako waliosahauliwa.
- Bwana, tunawaombea wale watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Tunaomba uwawezeshe kumruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi katika maisha yao
- Tunaomba pia kwa ajili ya mahitaji binafsi ya wale wote waliokusanyika hapa.

Shukrani

- Ahsante sana Mungu wetu kwa kutupatia ahadi nyingi kuhusu Roho Mtakatifu.
- Tunakushukuru kwa ajili ya ahadi iliyopo katika Luka 11:13 kwamba, “Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?”
- Tunakushukuru kwamba Roho wako Mtakatifu anatuongoza katika kweli yote.

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Njoo Roho Mtukufu (40); Ewe Roho wa Mbinguni (42); Nina Haja Nawe (126); Karibu na Wewe (152); Univute Karibu (148)

## MAFUTA YA UPAKO

Tazama, jinsi ilivyo vema, na kupendeza, Ndugu wakae pamoja, kwa umoja.Ni kama mafuta mazuri kichwani, Yashukayo ndevuni, ndevu za Haruni, Yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake. (Zaburi 133:1, 2)

**Mafuta yaliyotumika kuwapaka makuhani yalikuwa ni ishara ya Roho Mtakatifu. Tunahitaji Roho Mtakatifu, ndiye pekee anayeweza kuleta umoja katika kanisa letu ili tuweze kufanikiwa katika jitihada zetu za kimisionari.**

Maisha yetu ni lazima yafichwe ndani ya Mungu kupitia kwa Yesu Kristo. Ni lazima tuwe na uelewa binafsi wa Mungu, ndipo tunapoweza kumwakilisha kwa namna iliyo sahihi kwa ulimwengu. Ni lazima nuru yetu iangaze popote tulipo ikionesha utukufu wa Mungu kwa matendo yetu mema. Hii ndiyo kazi iliyo kubwa na muhimu katika maisha yetu. Wale ambao watakuwa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, watadhihirisha uwezo wake kwa kuweka katika uzoefu kanuni za kweli za milele. Wataonesha kwamba yale mafuta matakatifu yametolewa katika ile mizeituni miwili kuingia katika vyumba vya hekalu la nafsi. Maneno yao yatakuwa yamejawa na nguvu ya Roho Mtakatifu ili kulainisha na kutawala moyo. Itadhihirika kwamba maneno yanayosemwa ni roho tena ni uzima. (*Reflecting Christ,* uk. 130)

Yeye anayehisi udhaifu wake na akamenyana na Mungu kama Yakobo alivyofanya, kwa kulia kwamba, “Sitakuachia hata utakaponibariki,” ndipo patakuwepo na kupakwa upya kwa mafuta ya Roho Mtakatifu. Ndipo angahewa ya mbinguni itamzunguka, na mvuto na mguso wake utakuwa chanya sawa sawa na dini ya Kristo. (*Medical Ministry,* uk. 203)

Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. (Yohana 16:13)

Hebu na tuongezeke katika elimu ya kweli tukimsifu na kumtukuza yeye ambaye ni mmoja pamoja na Baba. Hebu na tutafute kwa dhati kupakwa mafuta ya mbinguni ambayo ni Roho Mtakatifu. Hebu tuwe na Ukristo safi unaokua, ili mwishowe kule katika vyumba vya mbinguni tupate kutamkwa wakamilifu katika Kristo. (*Reflecting Christ,* uk. 219)

Ni lazima pawepo na namna ya kubadilisha, kwa kuchukua na kuachia, kwa kupokea na kutoa. Kwa kufanya hivi, tunaunganishwa kama watumishi pamoja na Mungu.

Hayo ndiyo yanatakiwa kuwa ni maisha ya utendaji ya Mkristo, "yeye atakayeipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona."

Uwezo wa kupokea hayo mafuta matakatifu kutoka katika ile mizeituni miwili unaongezeka kadiri mpokeaji wa hayo mafuta anavoyatoa kutoka kwake kwenda kwa wengine kwa namna ya maneno au matendo ya kuwezesha roho zenye uhitaji. Kazi, yenye thamani, inayoridhisha itakayofanyika kwa kudumu kupokea na kutoa.

Tunahitaji, na ni lazima tupate mafuta mapya kila siku. Kwa kufanya hivi unadhani ni roho ngapi tunaweza kuzisaidia kwa kuwasiliana nazo? Mbingu yote inasubiri mifereji ambayo itatumika kupitishia mafuta ili kuleta furaha na mibaraka kwa wengine. Nina uhakika kwamba hakuna atakayefanya makosa ikiwa tu atakuwa mmoja pamoja na Kristo. Akiwa ndani yetu, tutafanya kazi bila kukoma kwa ukamilifu ili kazi hiyo tunayofanya ipate kudumu. Utimilifu wa kimbingu utamiminika kupitia kwa mawakala wa kibinadamu waliojitoa wakfu kuwafikia wengine. (*Testimonies for the Church,* vol.6 pp. 116, 117)

Roho Mtakatifu anapotawala fikra za washiriki wa kanisa letu, panakuwa na viwango vya juu sana vya hotuba, na huduma za kiroho kuliko inavyoonekana sasa. Washiriki watahuishwa na maji ya uzima, na watenda kazi wanaofanya kazi chini ya kiongozi ambaye ndiye kichwa yaani Yesu Kristo watamdhihirisha Bwana wao katika roho, katika maneno, matendo, na watatiana moyo wakisonga mbele katika kazi kubwa hii ya mwisho ambayo wameianza. Patakuwa na ongezeko la umoja na upendo lililo na afya, ambalo litakuwa na ushuhuda kwa ulimwengu kwamba Mungu alimtuma Mwana wake wa pekee ili afe kwa ajili ya ukombozi wa wenye dhambi. Ukweli wa kimbingu utainuliwa na kadiri unavyoangaza kama taa inayowaka, tutauelewa zaidi na kwa uwazi zaidi. (*Counsels for the Church*, uk. 100)

Tunakaribia mwisho wa historia ya ulimwengu huu, na Mungu anatuita wote kuinua viwango vyenye uvuvio. "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Anawaita watu wote wafanye kazi kwa upatanifu ulio kamili. Anawaita wale walio katika fani ya tiba kuunganika katika huduma; anaita huduma zote kushirikiana na huduma ya wamisionari wa kitabibu na analiita kanisa kutimiza wajibu wake, likiinua viwango vya matengenezo ya ukweli katika maeneo yao wakiwaacha wataalam na wenye uzoefu kuingia katika maeneo mapya. Tuepuke kutamka maneno yatakayowakatisha tamaa, kwani kwa kufanya hivi tunauhuzunisha moyo wa Kristo na kumfurahisha adui kwa sehemu kubwa. Wote wanatakiwa kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, wote tunatakiwa kuepuka kuawaona wengine kama

hawafai kwa kutoa kauli zinazokatisha tamaa na kuwafanya washindwe kumsogelea Kristo ili wapate kutambua uzito wa wajibu walio nao watendakazi pamoja naye. Maneno ya kiongozi wetu ni haya, "Sogeeni pamoja, jikusanyeni pamoja." Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. *(Counsels on Health*, uk. 517, 518)

SIKU YA PILI:

# MTAKATIFU KWA BWANA

**Fungu elekezi:** Mambo ya Walawi 20:26
"Nanyi mtakuwa watakatifu kwangu mimi; kwa kuwa mimi Bwana ni mtakatifu nami nimewatenga ninyi na mataifa, ili kwamba mwe wangu."

## MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA

### Kusifu

- Bwana tunakusifu kwa jinsi ulivyo – Wewe ni mwenye uwezo, hekima, rehema na ni mwenye upendo
- Tunakusifu kwamba umetuita kila mmoja wetu kuwa mtakatifu
- Tunakusifu kwa sababu una uwezo wa kutufanya sisi kuwa watakatifu.

### Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama hadharani na zile tunazotakiwa kuungama faragha. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhambi zetu.
- Utusamehe kwa nyakati tulizojaribu kushinda dhambi zetu kwa nguvu zetu wenyewe.
- Utusamehe kwani kuna nyakati ambazo tumeshindwa kudhihirisha tabia yako kwa wengine. Tunaomba utuwezeshe kufanya maisha yetu yaoneshe kwamba umetutenga na kwamba sisi ni mali yako.

### Kujitoa na Kufanya Maombezi

- Baba, tuoneshe jinsi ilivyo kuwa watakatifu. Tudhihirishie utakatifu wako.
- Tuoneshe jinsi ya kupambana kwa ajili ya "…huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao." (Waebrania 12:14)
- Bwana tunaomba kwamba, "nafsi zetu na roho zetu na miili yetu ihifadhiwe tuwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo." (1 Wathesalonike 5:23)
- Tunakuomba utuumbie moyo mpya kila mmoja wetu (Zaburi 51:10)
- Tafadhali utuoneshe jinsi tunavyoweza kukutukuza katika miili yetu. (1 Wakorintho 6:20)

- Tunaomba ubariki shirika la misaada la ADRA kadiri wanavyokabiliana na mahitaji ya masikini pamoja na wale waliosahauliwa.
- Bwana tunakuomba uimarishe imani yetu na kutuongoza katika kutenga muda wa kutosha kujifunza Biblia na kuomba. Hebu tutembee na wewe kila siku kama vile Henoko alivyotembea na wewe.
- Tunaomba ubadilishe mioyo yetu ielekee katika mambo ya umilele badala ya mambo ya dunia hii yanayovuta katika maovu. Tulinde kutoka katika mivuto ya kidunia ambayo inatishia uzoefu wetu wa kiroho wa kila siku
- Baba, mapenzi yako na yatimizwe katika maisha yetu na katika kanisa letu badala ya mapenzi yetu. Tunyenyekeze na kutufanya tunaofundishika tukiwa tayari kukumbatia mipango yako.
- Bwana, tunawaombea wale watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Tunaomba uwawezeshe kufungua mioyo yao ili uwafanye watakatifu
- Tunaomba pia kwa ajili ya mahitaji binafsi ya wale wote waliokusanyika hapa.

Shukrani

- Bwana, tunakshukuru kwamba tumeoshwa, tukatakaswa na kuhesabiwa haki "…katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu." (1 Wakorinto 6:11)
- Ahsante kwamba ulitupatia mioyo mipya (Ezekieli 36:26)
- Tunakushukuru kwamba tumetakaswa kwa Neno lako (Yohana 17:17)

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Ni Wako Bwana (144); Hasha Maneno Mabaya (150); Kuwa Wake Yesu (149); Bwana Ninataka Hili (116); U Mtakatifu (1)

## MTAKATIFU KWA BWANA

Nanyi mtakuwa watakatifu kwangu mimi; kwa kuwa mimi Bwana ni mtakatifu nami nimewatenga ninyi na mataifa, ili kwamba mwe wangu. (Mambo ya Walawi 20:26)

"Mtakatifu kwa Bwana" ndiyo chapa iliyokuwa katika kofia aliyovaa Kuhani Mkuu. Bwana anatutaka sisi, kama alivyowataka makuhani wa wakati ule wa kale kuishi maisha yaliyotengwa, maisha matakatifu. Maisha yetu yanatakiwa kumshuhudia yeye.

"Naye huyo akajibu, akawaambia wale waliosimama mbele yake, akisema, 'Mvueni nguo hizi zenye uchafu.' Kisha akamwambia yeye, 'Tazama, nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi.' Nikasema, 'Na wampige kilemba kizuri kichwani pake.' Basi, wakampiga kilemba kizuri kichwani pake, wakamvika mavazi; naye malaika wa Bwana akasimama karibu (Zakaria 3:4, 5)

Bwana hakukana mashtaka yaliyoletwa kuhusu kutokustahili kwa Yoshua, lakini alionesha kuwa amemnunua kwa thamani kubwa. Alimvika vazi lake la haki, sio kwamba alimvika vazi hilo juu ya mavazi yake machafu ya kutokutii na ukengeufu, bali kwanza alisema: 'Mvueni nguo hizi zenye uchafu.' Ndipo aliposema: "Tazama, nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi." Nikasema, 'Na wampige kilemba kizuri kichwani pake.' Basi, wakampiga kilemba kizuri kichwani pake, na kilemba kile kilikuwa na maandishi haya "Mtakatifu kwa Bwana." (*Manuscript Releases,* vol. 20, pp. 190, 191)

Mkristo anatakiwa kusimama kama mwakilishi wa kanuni za mbinguni. Anafungwa na wajibu mtakatifu kuwakilisha ukweli kwa sifa njema na upendo. Maneno yake na matendo yake na yawe na alama za upole, wema, na ukweli usiotiliwa mashaka wala kupinda. Akiwa amewekwa wakfu kwa Mungu na kutengwa kwa ajili ya huduma yake siku zote ataheshimu imani ya dini yake. Katika tabia yake hautaonekana unyuzi hata mmoja wa ubinafsi. Tunatakiwa kujifundisha kudhihirisha Roho wa Mungu katika utendaji wote wa maisha yetu. Kamwe Roho wa Mungu hawezi kuongoza hatua za watoto wake mahali pasipofaa. Tunaweza kupalilia na kuondoa kila jambo linaloleta maswali katika maisha yetu kupitia katika uwezo ambao Roho Mtakatifu anatoa. Ikiwa tutatoka katika giza linalofunika nafsi, na kuweka maisha yetu penye nuru inayong'aa ya Neno la Mungu, hiyo nuru itatuangazia na kutuongoza hatua kwa hatua katika mapito yanayoelekeza kwenye utakatifu. (*This Day with God*, uk. 281)

Tangu milele Mungu alichagua watu wawe watakatifu. "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu." Mwangwi wa sauti yake unatujia daima ukisema, "Mtakatifu, mtakatifu zaidi." Na jibu letu daima liwe, "Naam, Bwana, mtakatifu zaidi."

Hakuna anayeweza kupata utakatifu kama unavyopata haki ya kuzaliwa, au kama zawadi kutoka kwa mwanadamu mwenzake. Hii ni zawadi ya Mungu kupitia kwa Yesu Kristo. Wale ambao watampokea Mwokozi, wanahesabiwa kuwa wana wa Mungu. Hawa wamekuwa watoto wake kiroho, wamezaliwa upya, wamebadilishwa katika haki na utakatifu wa kweli. Fikra zao zimebadilishwa. Wakiwa na maono dhahiri wanautazamia uhalisia wa umilele. Wamekubaliwa katika familia ya Mungu,

na wamekuwa sawa na mwonekano wake kwa kubadilishwa na Roho kutoka utukufu hadi utukufu. Walikuwa wanatunza upendo wa ubinafsi, lakini sasa wanadhihirisha upendo mkuu kwa Mungu na kwa Kristo. (*Signs of the Times*, Dec. 17, 1902).

Mwokozi wetu ni Mwokozi anayemkamilisha mwanadamu kwa utimilifu wote. Sio Mungu wa sehemu ya ubinadamu tu. Neema ya Kristo inafanya kazi ikinidhamisha kila kipengele cha ubinadamu. Yeye ndiye aliyefanya yote, ndiye atakomboa yote. Yeye ndiye aliyeumba akili, nguvu, mwili hata na nafsi ambayo ndiyo yenye asili ya kimbingu, na kila kitu ni vya kwake lakini alivinunua tena vikawa ni mali yake. Ni lazima atumikiwe kwa akili zote, kwa moyo wote kwa roho yote na kwa nguvu zote. Ndipo Bwana atakapotukuzwa kati ya watakatifu wake na hata kati ya watu wa kawaida, pamoja na vitu vya kupita hivi ambavyo wameunganishwa navyo. Chapa ya "Utakatifu ni kwa Bwana" itaonekana imewekwa juu yao. (*God's Amazing Grace*, uk. 230)

Ikiwa kuna watu wanajaribu kuboresha fursa zao na kuwa na hekima na utendaji ulio mzuri, basi wale wanaotumia uwezo wao katika kujenga ufalme wa Mungu katika ulimwengu huu wangekuwa wa kwanza. Ukichukulia kwamba tunaishi katika nyakati ambazo karibu historia ya ulimwengu huu itafungwa, ni lazima pawepo na umakini katika utendaji kazi, kusubiri kwa matazamio, kukesha, kuomba na kufanya kazi. Huduma zote za kidini na nyanja zote za biashara ni lazima ziwe na chapa ya mbinguni. "Utukufu ni kwa Bwana" na liwe ndilo tamko la watendakazi kila idara. Kila wakala wa kibinadamu na ahangaike ili kupata ukamilifu, na kwamba aoneshe mfano mwema wa Ukristo, akikamilika katika Kristo Yesu. (*Review and Herald,* Oct. 5, 1905)

"Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu." (1 Petro 1:15, 16)

SIKU YA TATU:

# MIGUU ILIYO WAZI

**Fungu elekezi:** Kutoka 3:5

"Naye akasema, Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu."

**MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA**

**Kusifu**

- Bwana tunaanza kwa kukusifu kwa jinsi ulivyo – tabia yako na upendo wako wa kimbingu havipimiki
- Tunakusifu kwa ajili ya mfano wa Yesu ambaye aliuvaa ubinadamu
- Tunakusifu kwa "Maana wewe uliye juu, uliyetukuka, ukaaye milele; ambaye jina lako ni Mtakatifu; umesema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu. (Isaya 57:15)

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama faragha. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhambi zetu.
- Utusamehe kwa nyakati ambazo tumekosa kuwa na mioyo ya unyenyekevu.
- Utusamehe kwani kuna nyakati ambazo kiburi chetu hakikutuachia tukiri hatia yetu na kukuhitaji.

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Baba, tuoneshe jinsi ilivyo kunyenyekea chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili utukweze kwa wakati wako; ( Petro 5:6)
- Tuoneshe jinsi ya kujitia nira yako, tujifunze kwako; kwa kuwa wewe ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; ili tupate raha nafsini mwetu; (Mathayo 11:29)
- Tunakuomba utuoneshe maeneo ya maisha yetu tunapotakiwa kujifunza unyenyekevu
- Bwana, tafadhali inua watu wenye hofu yako, viongozi wanyenyekevu ambao wataonesha tabia ya Kikristo kwa maneno na matendo yao. Na utuoneshe jinsi

ya kutegemeza viongozi wetu kwa maombi, kuwatia moyo na kuwa tayari kutumika nao

- Tunaomba kanisa lako litangaze ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14 kwa uaminifu na kwa ukamilifu wake. Tupatie hekima ya kuifanya haki ya Kristo iwe ndiyo kiini cha ujumbe huu.
- Bariki jitihada zetu kadiri tunavyopanga "Vituo vya Mvuto" katika miji mikubwa duniani. Tupatie uwezo wa kuona na kupambanua sehemu zenye uhitaji katika kila mji. Tupatie ubunifu wa kuweza kukabiliana na mahitaji ya sehemu husika. Tuoneshe jinsi ya kuwaongoza wengine katika Neno lako kwa upendo.
- Bwana tunaomba utupe uamsho na maengenezo katika maisha yetu wenyewe, katika familia zetu, kanisani kwetu, na katika jamii yetu kwa ujumla. Tunakuomba uanze kwa kubadilisha mioyo yetu ili kwamb neema iweze kumiminika kupitia kwetu kwenda kwa wengine.
- Bwana tunaomba uguse Waadventista wa Sabato kote ulimwenguni wapate kuomba kwa namna ambayo hawajahi kuomba. Tuwezeshe kuomba na kusihi kwa pamoja kwa ajili ya kumwagwa kwa mvua ya masika ya Roho Mtakatifu. Tunaomba utimize ahadi yako iliyopo katika Yoeli 2, Hosea 6 na Matendo 2.
- Bwana, tunawaombea wale watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Tunaomba uwawezeshe kujinyenyekeza na kumruhusu Roho Mtakatifu kuwafundisha.
- Tunaomba pia kwa ajili ya mahitaji binafsi ya wale wote waliokusanyika hapa.

Shukrani

- Bwana, tunakushukuru kwa ajili ya ahadi hii: "Wenye upole utawaongoza katika hukumu, Wenye upole utawafundisha njia yako." (Zaburi 25:9)
- Ahsante kwa ajili ya Yesu ambaye, "alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." (Wafilipi 2:8)
- Tunakushukuru kwamba, "kabla ya heshima hutangulia unyenyekevu." (Mithali 15:33)

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Nina Haja Nawe (126); Yote Namtolea Yesu (122); Kumtegemea Mwokozi (129); Mahali pa Maji (181); Pana Mahali Pazuri Mno (180)

## MIGUU ILIYO WAZI

Naye akasema, Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. (Kutoka 3:5)

**Mungu alimwonya Musa asikaribie bila kicho. Kitendo cha kuvua viatu kinaashiria mwonekano wa heshima ambao ni muhimu katika ibada ya kweli.**

Mwonekano wa unyenyekevu na kicho unatakiwa kuonesha mwenendo wa wote wale wanaosogelea uwepo wa Mungu (*Patriarch and Prophets,* uk. 252)

Tunaweza kuja kwake kwa kujiamini kwa jina la Yesu, lakini tusimsogelee kwa kiburi kana kwamba tupo ngazi moja naye. Wapo wale ambao wanamchukulia Mungu mkuu mwenye uwezo wote, akaaye mahali pa juu pasipofikika kwenye nuru ya ajabu isiyoweza kupenyeka, kama mwenza wao au aliye duni kuliko wao. Wapo wale ambao wanapachukulia mahali pa kuabudia kama vile wako mbele ya wafalme wa dunia hii tu. Mungu ni mkuu anayestahili kuheshimika kwa hali ya juu, wote ambao wanatambua kwa dhati uwepo wake, watasujudu kwa unyenyekevu mbele yake. (*Patriarch and Prophets,* uk. 252).

Kule kuvikwa na hali ya unyenyekevu hakumaanishi kwamba tutageuka na kuwa wadumavu kiakili, tukapungua katika matarajio, na kuwa waoga maishani tukikwepa mizigo kwa kuogopa kuibeba kwa mafanikio. Unyenyekevu wa kweli unatimiza kusudi la Mungu kwa kutufanya tutegemee uweza wake (*God's Amazing Grace* uk. 270).

Lakini anatujalia neema zaidi. Kwa hiyo anasema, "…Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu." (Yakobo 4:6)

Mungu anafanya kazi kupitia kwa yeye anayemtaka. Wakati mwingine anachagua vyombo dhaifu lakini vinyenyekevu ili kufanya kazi kubwa, kwani uweza wake unadhihirishwa katika udhaifu wa wanadamu. Tunavyo viwango vya kibinadamu ambavyo vinatuwezesha kutamka kitu kimoja kuwa kikubwa na kingine kuwa kidogo; lakini Mungu hakadirii kulingana na viwango na kanuni za kibinadamu. Hatutakiwi kudhani kuwa kile kilicho kikubwa kwa viwango vyetu basi kitakuwa kikubwa mbele za Mungu, au kile kilicho kidogo kwetu kitakuwa kidogo mbele zake.

Kujisifu kunaokoonekana kwa wanadamu hakuna nafasi mbele zake… Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira hauhesabiwi kwa matendo yake mtu yeyote asije akajisifu, bali ihesabiwe kuwa ni neema

Hakuna dini ambayo inajitawalisha yenyewe, yeye anayefanya kujitukuza kuwe ndilo lengo lake, mwisho wake atajikuta akikosa neema ambayo ingemfanya kuwa bora katika kazi ya Kristo. Pale kiburi na kujiona bora kunapo tawala maisha, kazi inaharibiwa.

Mkristo ambaye katika maisha yake anajitoa kila siku na kuondoa ubinafsi, akiwa na kusudi la dhati kwa usafi wa fikra, akionesha unyenyekevu anaposhambuliwa, kwa imani na kicho, katika uadilifu kwa kila hali, yeye ambaye anawakilisha tabia ya Kristo nyumbani kwake, huyo atakuwa wa thamani machoni pa Mungu kuliko mmisionari mwingine wa aina yoyote au hata mfia dini. (*God's Amazing Grace* uk. 270).

"Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake." Mbingu yote inaingia katika ubia na wale wanaokuja kwa Kristo kwa ajili ya maisha ya milele, wakijitoa kwake kana kwamba wamekabidhi yote kwa Mungu. Mungu anahitaji watumishi wake wasimame chini ya bendera yenye damu ya Mfalme Emanueli, wakipambana kwa uweza wake kuhakikisha misingi ya kweli inabakia safi bila kuchafuliwa. Hawapaswi kuepuka mapito ya kujikana nafsi na unyenyekevu ambayo ni lazima Mkristo wa kweli ayapitie. Kadiri wanavyoshirikiana na Mungu, basi Kristo anaumbika ndani yao ambaye ni tumaini la utukufu. Wakijitoa kikamilifu katika unyenyekevu na kujishusha, wanapitia katika uzoefu wa furaha isiyo na kipimo kwa kushiriki katika huduma yake. Mivuto ya kidunia inatoa nafasi kwa haja ya kumtumikia Bwana. (*Review and Herald*, May 11, 1897, aya ya 14)

Tunahitaji kumsogelea Mungu ili tuone kama kuna vitendo vya wivu au kijicho vinazokuzuia kuelekea kwa Mwokozi. Ubinafsi, na kujiona kuwa unajitosheleza hufunga mlango wa moyo dhidi ya Yesu, na kusema "Sihitaji mapito yako, nitafuata njia zangu." "Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake." Toba ya dhati inayotoka moyoni, kutoka katika moyo uliofanywa mgumu kwa anasa za ulimwengu huu itasikiwa na Mungu, na dhambi zote zitaonekana kwa mhusika jinsi zinavyoonekana machoni pa Mungu aliye Mtakatifu. (*Testimonies to Southern Africa*, uk. 78)

Mungu anao watu wake aliowachagua atakaowatumia katika kazi yake ikiwa watamruhusu awatumie kama apendavyo. Hawezi kumtumia tu yeyote anayetaka kumnyenyekeza mwingine. Ndugu zangu tujinyenyekeze mbele zake, unapofanya hivi, malaika watakatifu wanaweza kuwasiliana nawe na kukuweka mahali palipoinuka. Ndipo uzoefu wako utajazwa na furaha badala ya kusikitika. Tafuta uhusiano wa

upatanifu na Mungu ili akuongoze, ndipo utakapopata hisia za kuguswa na Roho Mtakatifu. (*North Union Gleaner*, March 23, 1910, aya ya 5)

SIKU YA NNE:

## JOHO

*(LA KUHANI)*

**Fungu elekezi**: Isaya 61:10
"Nitafurahi sana katika Bwana, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; maana amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki …)

### MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA

**Kusifu**

- Mungu wetu tunakusifu kwa jinsi ulivyo – wewe ni mwenye haki, safi na mwenye uwezo
- Tunakushukuru kwa kukubali kutupatia vazi la Kristo la haki.
- Tunakusifu kwa kuwa "…kazi ya haki itakuwa amani; na mazao ya haki yatakuwa ni utulivu na matumaini daima." (Isaya 32:17)

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama kwako.
- Tusamehe hasa nyakati ambazo tumevaa mavazi ya haki yetu wenyewe badala ya kujivika vazi la haki ya Kristo
- Utusamehe ile hali yetu ya kujiona kwamba tunajitosheleza.

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Baba, tafadhali tuongoze kulikubali vazi la haki ya Kristo
- Tusaidie kufahamu kuwa, "…sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi; sisi sote twanyauka kama jani, na maovu yetu yatuondoa, kama upepo uondoavyo. (Isaya 64:6). Utusaidie kuiona haki yetu wenyewe kwa jinsi unavyoiona wewe.
- Tunakuomba utufundishe jinsi ya "kuzikimbia tamaa za ujanani; tukafuate haki, na imani, na upendo, na amani." (2 Timotheo 2:22)
- Tafadhali tufundishe jinsi ya "kutokuenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho." Ili kwamba matakwa ya sheria ya haki yapate kutimizwa ndani yetu. (Warumi 8:4)
- Tafadhali panda ndani yetu tunda la haki

- Tafadhali uwalinde vijana wetu kutoka katika majaribu ya dunia hii, geuza macho yao yamwelekee Yesu
- Baba, tafadhali tufundishe kushiriki na wengine mkate wa uzima. Tupatie nguvu tunapokuwa wadhaifu. Hofu inapotuinga, tupatie ujasiri.
- Tunaomba utupatie mtazamo mpya kuhusu kusoma vitabu vya Danieli na Ufunuo pamoja na vitabu vingine vya unabii. Wapatie washiriki wetu tumaini imara la mambo yajayo na uelewa dhahiri kuhsu pambano kati ya Kristo na Shetani.
- Bwana tufundishe jinsi ya kujifunza Neno lako kila siku sisi wenyewe. Tupatie msukumo wa kushiriki katika program ya "Amini Manabii Wake" kwa kusoma Biblia na vitabu vya Roho ya Unabii pamoja kama kanisa la ulimwengu.
- Tusaidie kila mmoja wetu kuthamini na kutafuta hekima iliyovuviwa iliyotolewa kwa kanisa letu katika maandiko ya Roho ya Unabii. Hebu mashauri haya yatuongoze katika Neno lako kwa undani.
- Bwana, tunawaombea wale watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Tunaomba kwamba Roho Mtakatifu abadilishe mioyo na fikra zao.
- Tunaomba pia kwa ajili ya mahitaji binafsi ya wale wote waliokusanyika hapa.

**Shukrani**

- Bwana, tunakshukuru kwa kuwa wote wanaotamani haki ya Kristo wanaweza kuipata bure kabisa
- Ahsante kwa ajili ya maisha na kifo cha Yesu ambacho kinatuwezesha kuifikia haki yako.

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Yesu Mwokozi (51); Ulimwengu Siutaki (145); Njiani Huniongoza (155); Mwokozi Kama Mchunga (18); Mchungaji Mpenzi (105)

## JOHO *(LA KUHANI)*

Naye akasema, Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo

**Joho ni ishara ya haki ya Kristo inayofunika uchi wetu pale tunapoikubali.**

Wale wote waliojivika vazi la haki ya Kristo watasimama mbele zake kama waliochaguliwa, waaminifu na wakweli. Shetani hana nguvu tena kuwang'oa kutoka mikononi mwa Kristo. Hakuna roho itakayokuwa katika majuto ya dhati, itakayodai

ulinzi wake na kuachiwa chini ya uweza wa adui. Neno lake limeahidi kuwa, "Au azishike nguvu zangu, Afanye amani nami; Naam, afanye amani nami." (Isaya 27:5). Ahadi aliyopewa Yoshua ni kwa ajili yetu wote: "Kama ukienda katika njia zangu, na kama ukishika maagizo yangu, ndipo utakapoihukumu nyumba yangu, nawe utazilinda nyua zangu, nami nitakupa nafasi ya kunikaribia kati yao wasimamao karibu." (Zekaria 3:7). Malaika wa Mungu watatembea pande zote, hata ulimwenguni humu, mwishowe watasimama kati ya malaika wanaozunguka kiti cha enzi cha Mungu. (*Counsels for the Church*, uk. 351, 352)

Ni haki ya Kristo ndiyo inayomfanya mwenye dhambi aliyetubu kukubaliwa mbele za Mungu kwa kazi yake ya kuhesabiwa haki. Bila kujali jinsi maisha yake yalivyojawa na dhambi, akimwamini Yesu kama Mwokozi wake binafsi, atasimama mbele za Mungu akiwa amevikwa vazi la haki ya Kristo lisilo na doa. (*Faith and Works*, uk. 106)

"Tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani." (Wafilipi 3:9)

Mwenye dhambi ambaye ni mfu katika dhambi anahuishwa kwa imani katika Kristo. Kwa imani anaona kwamba Yesu ni Mwokozi wake, na anaishi milele akiwa na uwezo wa kuokoa wale wote wanaokuja kwa Mungu kupitia kwake. Mwenye dhambi anaona mapana na marefu na kina cha ubora katika upatanisho uliofanywa kwa ajili yake. Anaona ukamilifu wa wokovu, akiwa amenunuliwa kwa gharama isiyopimika, ndipo nafsi yake inajawa na sifa na shukrani. Anaona utukufu wa Bwana kupitia katika kioo na anabadiliswa na kufanana naye kama vile katika roho ya Bwana. Analiona vazi la haki ya Kristo likiwa limefumwa kwa chombo cha mfumaji cha mbinguni kwa nyuzi za utii, ili kumwezesha yeye aliyeungama kupitia kwa imani katika jina lake.

Pale mwenye dhambi anapoona furaha ya Yesu, dhambi inakoma kuonekana nzuri kwake, kwani anakuwa amemtazama mkuu katika maelfu, yeye ambaye anampenda. Ndipo anapotambua kwa uzoefu binafsi wa nguvu ya injili, ambayo upeo wake wa ubunifu unalinganishwa tu na makusudi yake. (*Faith and Works,* uk. 106, 107).

Kadiri watu wa Mungu wanavyopitia katika maumivu mioyoni mwao, wakililia usafi wa mioyo, agizo linatolewa kwamba, "Mvueni nguo hizi zenye uchafu." Na maneno ya kutia moyo yanatamkwa kwamba, "Tazama, nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi." Yule aliyechoka kwa majaribu na akawa mwaminifu wa Mungu anavishwa vazi lisilo na doa la haki ya Kristo. Wale walio

masalia ambao walibezwa, sasa wanavikwa vazi la utukufu, wasije tena wakachafuliwa na uharibifu uliomo ulimwenguni. Majina yao yanabakizwa kwenye kitabu cha uzima cha Mwana Kondoo yakiwa yameorodheshwa pamoja na waaminifu wengine wa vizazi vyote. Wamekataa vishawishi vya Yule mdanganyifu, hawakuondolewa kutoka kwenye uaminifu kwa kuunguruma kwake simba. Sasa wako salama milele, wapo ng'ambo ya mbinu zote za yule mjaribu. Dhambi zao zimehamishiwa kwa yule mwanzilishi wa dhambi. (*Counsels for the church,* uk. 353)

Imani ya kawaida tu haitoshi. Ni lazima tujivike vazi la haki ya Kristo na kulivaa wazi wazi, kwa ujasiri tukiwa tumedhamiria, tukimdhihirisha Kristo bila kutazamia chochote kutoka kwa mwanadamu, tukimtazama Yesu ili tupate kufananishwa na ukamilifu wake wa tabia. Ndipo kila mmoja wetu atadhihirisha tabia ya Yesu na kuonesha kwamba tumejawa na kweli; kwa sababu kweli inatakasa nafsi na kuteka kila fikra ipate kumtii Kristo. (*Reflecting Christ*, uk. 108)

Wale ambao kwa kweli ni wenye haki, ambao wanampenda na kumheshim Mungu kwa dhati watavaa vazi la haki ya Kristo ima kwa mafanikio au kwa mateso. Kujikana nafsi, kujitoa kafara, kutenda wema, upendo, ustahimilivu, kudhamiria na imani ya Kikristo ndiyo matunda ya kweli ya kila siku yanayooneshwa na wale ambao kwa kweli wameunganika na Mungu. Inawezekana matendo yao yasifahamike kabisa duniani, lakini wao wenyewe wanapambana na uovu kila uchao, huku wakishinda majaribu na mabaya yanayojitokeza. (*God's Amazing Grace*, uk. 31).

"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa." (1 Petro 2:24)

Kila mmoja atakabilana na pambano ili kushinda dhambi ndani ya moyo wake mwenyewe. Wakati mwingine zoezi hili linaweza kuwa chungu na la kukatisha tamaa kwa sababu mara nyingi tunajaribiwa kuelekeza fikra zetu katika mapungufu ya tabia zetu badala ya kumwangalia na kujivika vazi la haki yake. Kila mmoja atakayeingia katika malango ya lulu ya ule mji wa Mungu, ataingia kama mshindi, na ushindi wake mkuu utakuwa ni ushindi dhidi ya nafsi. (*God's Amazing Grace*, uk. 31)

"Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake." (Zaburi 23:3)

SIKU YA TANO:

# NAIVERA

**Fungu elekezi: Isaya 46:4**
"Na hata uzee wenu mimi ndiye, na hata wakati wenu wa mvi nitawachukueni; nimefanya, nami nitachukua; naam, nitachukua na kuokoa."

## MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA

**Kusifu**

- Bwana, tunaanza kwa kukusifu kwa jinsi ulivyo – wewe ni imara, mvumilivu, na una uwezo wa kuokoa
- Tunakushukuru kwa kutupitisha katika nyakati zilizokuwa ngumu sana kwetu.
- Tunakushukuru kwa kuwa hatimaye tuna amani ya kudumu na furaha katika wewe.

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama hadharani na zile ambazo tunatakiwa kuungama kwa faragha. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhmabi.
- Tusamehe hasa nyakati ambazo tumetafuta kushinda kwa uwezo wetu badala ya kukuruhusu ushinde ndani yetu
- Ahsante kwa sababu unatusamehe kulingana na 1 Yohana 1:9.

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Bwana, tuinue tunapokuwa dhaifu
- Hebu uweza wako ukamilike katika udhaifu wetu (1 Wakorintho 12:9)
- Baba, tusaidie mioyo yetu isifadhaike. (Yohana 14:1)
- Tusaidie kuamini ahadi uliyoitoa katika Isaya 41:10 – kwamba, "usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu."
- Tafadhali washikilie vijana waliopo katika makanisa yetu na familia hasa nyakati hizi za mashaka.
- Tuoneshe watu wanaotuzunguka ambao inawezekana wanapitia katika maumivu ya aina fulani. Wavushe katika changamoto wanazopitia.

- Bwana tuoneshe jinsi ya kutoa maisha yetu kikamilifu kwako. Tufanye tuwe kitu kimoja na Kristo, tuunganishe katika kutangaza ujumbe wa mwisho wa kilio kikuu kwa ulimwengu unaotuzunguka.
- Bwana umelibariki kanisa letu kwa uelewa mkubwa wa ukweli wa Biblia, tunakuomba utuwezeshe kuushiriki ukweli huu kwa unyenyekevu na ulimwengu unaotuzunguka.
- Baba, tafadhali bariki jitihada za vikundi vidogo na makanisa yaliyo kwenye nyumba za watu kote ulimwenguni. Tunakuomba uinue washiriki waaminifu watakaoshuhudia kumhusu Yesu Kristo na tabia yake nzuri kwa majirani wao.
- Bwana tufundishe jinsi ya kutangaza misingi ya imani ya kanisa letu kwa uwazi na ubunifu utokao katika umahiri wa Biblia. Hebu upendo wa Kristo uwe ndio kiini cha mambo yote tunayoamini.
- Bwana, tunawaombea wale watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Tunaomba kwamba uwawezeshe kuona mahitaji yao na kufungua mioyo yao kwa Roho Mtakatifu.
- Tunaomba pia kwa ajili ya mahitaji binafsi ya wale wote waliokusanyika hapa.

**Shukrani**

- Bwana, tunakshukuru kwamba, "wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia." (Isaya 40:31)
- Ahsante kwa kuwa "katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake." (Warumi 8:28)
- Tunakushukuru kwa kuwa unajibu maombi tunayoomba kulingana na mapenzi yako.

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Miguuni Pake Yesu (46); Yesu anasema (119); Yanipasa Kuwa Naye (154); Mwokozi Kama Mchunga (18); Unifundishe Baba (136)

## NAIVERA

"Na hata uzee wenu mimi ndiye, na hata wakati wenu wa mvi nitawachukueni; nimefanya, nami nitachukua; naam, nitachukua na kuokoa." (Isaya 46:4)

Kwa namna ambavyo kuhani mkuu alivyobeba ile naivera katika mabega yake, ndivyo Kuhani Mkuu anavyobeba mizigo yetu, akitutegemeza na kutuimarisha katika majaribu yanayotukabili na kutuwezesha kumshuhudia hata katika mazingira magumu.

Mwokozi wetu wa thamani ametukaribisha kujiungamanisha kwake na kuunganisha udhaifu wetu kwenye Uwezo Wake, kutokujua kwetu katika Hekima yake, kutokustahili kwetu katika kustahili kwake. (*The Faith I Live By*, uk. 96)

“Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.” 1 Petro 5:7

Kwa wale waliovunjika mioyo kuna msaada – imani, maombi, kazi, na kujishughulisha kutawezesha kupata uhakika na kuridhika ambako kutaongezeka siku kwa siku. Je unajaribiwa kujiachia katika fikra na hisia za kukata tama? Katika siku ambayo unaona giza, unapoona kila kitu hakiko upande wako, usiogope. Mwamini Mungu tu. Anafahamu kile unachohitaji, na hatabadilisha agano lake kwa wale wampendao. Naye atawajalia watumishi wake waaminifu kipimo cha ubora wanachohitaji. Mtume Paulo anashuhudia kwamba, “Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu.” (2 Wakorintho 12:9, 10). *Prophets and Kings*, uk. 164

Nguvu za wale ambao wanampenda na kumtumikia zitaongezwa na kufanywa upya siku hadi siku. Ufahamu wake utakuwa juu yao katika kazi yake ili wasikosee katika kutimiza kusudi lake. Sio vema kukata tama katika kazi ya Mungu. Imani yetu inatakiwa kustahimili msukumo unaojitokeza. Mungu anaweza na yupo tayari kuwapatia watumishi wake nguvu wanayohitaji. Atatimiza matazamio yao kwa upeo wa juu kuliko wanavotazamia wale wanaoweka matumaini yao kwake. Atawapatia hekima wanayohitaji katika utendaji mbali mbali. (*Testimonies for the Church*, vol. 8 uk. 10, 11)

Sisi wenyewe hatuwezi kupata au kufanyia mazoezi dini ya Kristo kwa sababu mioyo yetu ni midanganyifu kuliko vitu vyote, ila Yesu ambaye ni tabibu mkuu wa roho zetu, ambaye ana ustadi usiokosea, ndiye anayeweza kusoma mioyo ya wanadamu kuliko wao wenyewe, ametuonesha jinsi tunavyoweza kusafishwa kutoka katika dhambi. Kwa wale ambao wanahuzunikia ukosefu wa ubora, anasema “Neema yangu yakutosha,”

kisha anasema "Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha." Yeye anafahamu mizigo hiyo kabla hata haijawekwa mabegani mwetu. Yesu anaiambia kila roho iliyojaribiwa kwamba, nipo tayari kukuimarisha kwa ajili ya majukumu ya maisha ya Kikristo. Tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; tutaangazwa na nuru kutoka katika paji la uso wake, itakayoakisi sura yake na kutufanya tukue na kufikia utimilifu wa kimo cha wanaume na wanawake katika Kristo Yesu. Dini yetu itavutia kwa sababu itanukia manukato ya haki ya Kristo. Tutafurahi kwa sababu chakula chetu na kinywaji chetu kitakuwa ni haki yake na amani na furaha. (*Review and Herald,* May 4, 1897, aya ya 11).

Ni jambo kubwa, tena jema ukiwa na uhusiano mzuri na Mungu, roho zetu kuwa na upatanifu na Muumba wetu. Malaika watatumwa kuokoa kutoka kati kati ya mifano ya uovu inayoambukiza, ambayo kwa udanganyifu wake unaoambukiza inaweza kushawishi roho kutoka katika wajibu. Lakini ikiwa tutakaribisha majaribu, hatuwezi kupata msaada wa kimbingu wa kutuwezesha kuyashinda. Wale vijana watatu walistahimili tanuru ya moto kwa sababu Yesu alitembea nao ndani ya ile miali ya moto. Kama wao wenyewe wangeingia ndani ya tanuru na kujaribu kutembea ndani ya moto, wangeungua mara moja. Ndivyo itakavyokuwa kwetu, ikiwa hatutaingia katika majaribu kwa makusudi tu, Mungu atatutegemeza pale majaribu yanapotukabili. (*Signs of the Times*, Sept. 2, 1897, aya ya 11)

Bwana anainua watu na kuwajaza Roho wake ndani yao akiwatayarisha kwa ajili ya kazi ambayo ni lazima ifanyike. Yeye mwenyewe ambaye ni Mungu wa kweli atawafanya wastahili kuwa ushuhuda ulio hai kwa ajili yake. Watakuwa mashahidi wa Mungu. Hawatajitokeza kwa msukumo wao wenyewe bali watashurutishwa na Roho wa Mungu kujitolea ili kutangaza ukweli. Mungu atawategemeza. Kila mwaka anaona kile kinachohitajika na kupanga mipango ya utendaji. Hatawaacha waende tu jinsi wanavyotaka. Ikiwa watu watakuwa tu ni watu, Mungu atatenda kazi ndani yao na kupitia kwao. (*Review and Herald,* May 25, 1897, aya ya 11)

SIKU YA SITA:

# MSHIPI

**Fungu elekezi:** 1 Petro 3:15

“Mwe tayari siku zote kumjibu kia mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.”

**MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA**

**Kusifu**

- Bwana tunaanza kwa kukusifu kwa jinsi ulivyo – tabia yako na upendo wako wa kimbingu havipimiki.
- Asante kwa nafasi ya pekee ya kuwa mashahidi wako.
- Tunakushukuru kwamba unapotuita tukutumikie, unatupatia pia nguvu na uwezo wa kufanya hivyo.

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama faragha. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhambi zetu.
- Utusamehe kwa nyakati ambazo hatukuwa tayari kukutumikia.
- Utusamehe kwa nyakati ambazo tulikataa kuwa mashahidi wako.

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Baba, tafadhali tupatie mioyo iliyo tayari kukutumikia.
- Tufundishe namna ya “kuiacha nuru yetu na iangaze mbele za watu, wapate kuyaona matendo yetu mema, wamtukuze Baba yetu aliye mbinguni” (Mathayo 5:16).
- Tafadhali tusaidie kuziona fursa za kukutumikia unazotupatia.
- Tunakuomba utupatie maneno sahihi ya kukushuhudia pale fursa zinapojitokeza.
- Bwana, tusaidie kumtumikia bwana mmoja tu (Mathayo 6:24).
- Tafadhali ruhusu familia zetu kudhihirisha upendo wako katika nyumba na jamii zetu. Tunakuomba ulete umoja katika nyumba zetu, ponya mahusiano yaliyovunjika, linda walio katika hatari ya unyanyasaji, na dhihirisha nguvu zako zitakasazo katika nyakati zinazoonekana kutokuwa na tumaini.

- Bwana, tunaombea maelfu ya waanzilishi wa utume ulimwenguni ambao wanaanzisha makanisa katika maeneo yasiyofikiwa. Wengi wao wanafanya kazi peke yao katika mazingira magumu kwa hiyo tunaomba kwa ajili ya usalama wao, uwahekimishe na kuwafanikisha.
- Bariki jitihada za Mtandao wa Wataalam wa Kiadventista. Wapatie fursa za kimbingu ili wafanye utume kwa wanataaluma na wasomi katika maeneo ya dunia yaliyopo mijini.
- Tunakuomba uwapatie ulinzi wa pekee washiriki wa kanisa wanaokabiliana na manyanyaso au vitisho kwa usalama wao kwa sababu tu ya imani yao. Tuaomba uwapatie hekima na ujasiri. Utuguse tupate kuishi kama mashahidi katika ulimwengu ambao haukufahamu.
- Bwana, tunamba kwa ajili ya watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Hebu wafungue maisha yao kwa Roho Wako Mtakatifu na wawe mashahidi wako.
- Pia tunaomba kwa ajili ya mahitaji binafsi ya waliokusanyika hapa.

**Shukrani**

- Bwana, tunakushukuru kwa kutengeneza tabia zetu kupitia huduma yetu kwako.
- Tunakushukuru kwa furaha inayotokana na kukushuhudia.
- Tunakushukuru kwamba Kristo ameshatupatia mfano wa namna ya kukutumikia.

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Nitakuandama Kote (138); Taa Yangu Ndogo (); Nitwae Hivi Nilivyo (140); Popote na Yesu (133); Namwandama Bwana (128)

## MSHIPI

"Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu." (1 Petro 3:15)

**Kwa kuhani mkuu kuweza kufungwa kwa mshipi wake ilimaanisha kwamba tayari alikuwa amevaa nguo zake zote, na yupo tayari kuhudumu. Vivyo hivyo, daima tunapaswa kuwa tayari kuhudumu na kushuhudia.**

Watu wa Mungu wanapaswa kutofautishwa kama watu wanaomtumikia wakati wote, kwa mioyo yao yote, wasiojichukulia heshima wenyewe, na wanaokumbuka kwamba agano la pekee kabisa ambalo wamejitoa kumtumikia Mungu, na Yeye peke yake. (*Christian Service,* uk. 236)

Kumtumikia Mungu kuna maana gani? – Ni kufanana naye katika tabia, kumdhihirisha. Kumtumikia Mungu, ni kumtii na kuzishika amri zake, kufanya ungamo la wazi la kusimama, si chini ya bango jeusi la yule muasi mkuu, lakini chini ya bango lenye damu ya Emanueli mwana wa Mfalme. Wale wanaomtumikia Mungu wanapambana kwa dhati kutii nia yake. Hivyo wanaonyesha kwamba ni jeshi gani wanalotumikia. (*Signs of the Times,* Feb. 1, 1889, aya. 3)

Katika kazi yoyote tutakayojihusisha nayo, neno la Mungu linatufundisha kutenda, "kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana." "Lolote mkono wako utakalopata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako zote," "mkijua ya kuwa mtapokwa kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo." Warumi 12:11; Mhubiri 9:10; Wakolosai 3:24. (*Christ Object Lessons,* uk. 346)

Daima uwe tayari kuwapatia wengine nuru uliyoipokea. Dhihirisha kanuni za matendo yako; dharau kuficha kile chema ulichopata. Kunjua rangi zako; kwani wewe ni miwani kwa ulimwengu, kwa malaika, na kwa wanadamu. Usikwepe majukumu. Huwezi kumtumikia Mungu na Baali. Mungu anatamani wana na binti zake kusimama kwa hekima katika kweli, ili kwamba ulimwengu uweze kufahamu upande watakaosimama wakati wa hukumu. (*Signs of the Times,* Agost. 1, 1900, aya. 4)

Bwana anatamani muwe watu wa kuongoa roho; kwa sababu hiyo msipende kulazimisha mambo ya kiroho kwa watu, bali "Mwe tayari siku zote kumjibu kia mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu." 1 Petro 3:15. Kwa nini uhofu? – ogopa kwamba maneno yako yanakufanya ufurahie kujiona bora, usitamke maneno yasiyofunikwa na ushauri, maneno yako na matendo yako yasikose kufanana na Kristo. Jiunganishe kikamilifu na Kristo, na uonyesha ukweli kama ulivyo ndani yake. (*Manual for Canvassers,* uk. 34)

"Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele za watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni." (Mathayo 5:16).

Mungu anatamani kila muumini awe muongoaji wa roho; na atawabariki wale wote wanaomtazama kwa ujasiri ili wapate hekima na uongozi. Kadiri wanavyotembea wakilindwa, wakitembea katika njia ya hekima, na kudumu kuwa wakweli kwa

Mungu wa Israeli, usafi na urahisi wa Kristo uliodhihirishwa katika uzoefu wa maisha, utashuhudia uwepo wa uchaji wa Mungu. Katika yote wanayosema na kutenda, watalitukuza jina la yule wanayemtumikia.

Muumini aliyejazwa na roho ya kweli ya umisionari, ni barua iliyo hai, inayofahamika na kusomwa na watu wote. Ukweli hutoka katika vinywa vyake bila maneno ya kujionyesha. Uchaji wake wa Mungu na ari pamoja na maamuzi yaliyotakaswa hukua kadri siku zinavyosonga, na dunia isiyoamini huona kwamba anaishi katika ushirika na Mungu akijifunza kutoka kwake. Maneno yanayonenwa na vinywa vilivyobadilishwa husindikizwa na nguvu inayogusa mioyo iliyo baridi ya wasioamini; hata wale wasiomfahamu Mungu wanaweza kutofautisha kati ya ubinadamu na uungu.

Ndugu na dada zangu, je, unaihisi nguvu ya utakaso ya ukweli mtakatifu katika moyo wako, na maisha yako, na tabia yako? Je, una uhakika kwamba Mungu, kwa sababu ya mwanawe wa pekee, amesamehe dhambi zako? Je, unapambana kuishi kwa dhamiri safi isiyo na hatia mbele za Mungu na mwanadamu? Je, unamsihi Mungu daima kwa niaba ya rafiki na jirani zako? Kama umefanya amani na Mungu, na umeweka yote juu ya madhabahu, unawea kujihusisha katika huduma ya kuongoa roho kwa faida. (*Manuscript Release,* vol. 8, pp. 212, 213)

Hebu maneno yetu na yawe ya upole kadri tunavyotafuta kuokoa roho. Mungu atakuwa hekima kwa yule anayetafuta hekima kutoka katika chanzo cha kimbingu. Tunapaswa kutafuta fursa kila mahali. Tunapaswa kukesha na kuomba, na kuwa tayari siku zote kumjibu kila mtu atuulizaye habari za tumaini lililo ndani yetu; lakini kwa upole na kwa hofu. Tusije tukawa na mguso mbaya kwa roho hata moja ambayo Kristo aliifia, tunapaswa kuinua mioyo yetu kwa Mungu, ili fursa inapojitokeza, tuweze kuwa na maneno sahihi ya kuzungumza kwa wakati muafaka. Hivyo unapojitoa kufanya kazi ya Mungu, Roho wake atakuwa msaidizi wako. Roho Mtakatifu atathibitisha ukweli uliozungumzwa kwa upendo kwa ajili ya nafsi hiyo. Ukweli utakuwa na nguvu ya kuwezesha utakapozungumzwa katika msukumo wa neema ya Kristo. (*The Publishing Ministry,* uk. 307)

SIKU YA SABA:

## KIFUKO CHA KIFUANI

**Fungu elekezi:** 1 Wakorintho 1:10

"Basi ndugu, nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja."

**MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA**

**Kusifu**

- Bwana, tunaanza kwa kukusifu kwa jinsi ulivyo – Wewe ni Mungu wa upendo, amani, na umoja.
- Tunakusifu kwa mfano wa umoja uliokuwepo kati ya wanafunzi wako baada ya Pentekoste.
- Tunakushukuru kwamba unaweza kuleta umoja katika makanisa na familia leo.

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama hadharani na tunazotakiwa kuungama faragha. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhambi zetu.
- Utusamehe kwa nyakati ambazo hatukuwa na umoja katika mwili wa Kristo kwa maneno na matendo yetu.
- Tunakushukuru kwamba unatusamehe kulingana na 1 Yohana 1:9.

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Baba, tafadhali wafanye watu wako "waufikilie umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo." (Waefeso 4:13).
- Tusaidie kutotenda jambo lolote "kwa kushindana wala kwa majivuno, bali kwa unyenyekevu, kila mtu na mahesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake" (Wafilipi 2:3).
- Bwana, tafadhali tupatie mioyo ya unyenyekevu na upendo kwa watu walio wagumu kuishi nao au kufanya nao kazi. bwana, tafadhali tuonyeshe kila mmoja wetu pale tunapozuia umoja katika mahusiano yetu ya kanisa au familia. Tafadhali lainisha mioyo yetu na tupatie umoja kulingana na mpango wako.

- Tunaomba kwa ajili ya umoja kati ya viongozi wetu wa makanisa mahalia na katika kanisa la ulimwengu.
- Tunaomba kila mshiriki wa kanisa la Waadventista wa Sabato duniani apate maono ya ushirikishwaji wa washiriki wote (TMI). Tuwezeshe kila mmoja wetu kuwa hai katika ushuhudiaji binafsi, na vikundi vidogo vidogo vinavyoifikia jamii au umma kwa uinjilisti.
- Tafadhali tuma Roho wako Mtakatifu atayarishe mioyo ya wasikilizaji wa Radio ya Waadventista wa Sabato ulimwenguni, hasa maeneo ya dunia yaliyoko mijini. Wajalie washiriki kuwa waaminifu kufuatilia na kuwafanya wale wanaokutafuta kuwa wanafunzi wako.
- Wabariki washirika wa kanisa letu kama shirika na kutegemeza huduma mbali mbali katika kazi yako kuu ya kuwafikia watu kwa uinjilisti. Wajalie watumishi wako kufanya kazi pamoja wakipendana kila mmoja na mwenzake huku wakikupenda wewe.
- Bwana tafadhali tuoneshe jinsi ya kupeleka vijuzuu vilivyojawa na kweli (vile vilivyochapishwa pamoja na kwenye mtandao) katika jamii inayotuzunguka. Inua wainjilisti wengi wa vitabu, wanafunzi wanaojitolea, waandishi, wataalam wa mitandao, na watu wenye fedha watakaotegemeza uenezaji wa Neno na tumaini la maisha ya milele.
- Bwana, tunaomba kwa ajili ya watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Wawezeshe kumruhusu Roho Mtakatifu afanye kazi katika maisha yao.
- Pia tunaomba kwa ajili ya mahitaji binafsi ya waliokusanyika mahali hapa.

**Shukrani**

- Bwana, tunakushukuru kwa ajili ya Yesu, aliyeomba kwa sababu ya umoja wetu katika Yohana 17
- Tunakushukuru kwamba umoja katika kanisa husaidia ulimwengu kuamini kwamba Yesu ndiye Mwana wa Mungu (Yohana 17:21).

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Mungu Wetu Yeye Mwamba (20); Upendo Ni Furaha (199); Si mimi, Kristo (17); Mungu Atukuzwe (3)

## KIFUKO CHA KIFUANI

"Basi ndugu, nawasihi kwa jina la Bwan wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja." 1 Wakorintho 1:10

**Mawe 12 yanayowakilisha makabila 12 ya Israeli yaliwekwa katika kifuko cha kifuani karibu na moyo wa Kuhani Mkuu. Kutoka katika hili tunajifunza ilivyo muhimu kwetu kusihi pamoja ili tuunganishwe katika upendo wa Kristo, na kudhihirisha upendo huo kwa watu, ndani na nje ya kanisa.**

Siri ya mafanikio yetu katika kazi ya Mungu itapatikana kwa watu wetu kufanya kazi kwa umoja. Lazima kuwepo na utendaji wa pamoja. Kila mshiriki wa kanisa la Kristo anapaswa kufanya sehemu yake katika kazi ya Mungu, kulingana na uwezo aliopewa na Mungu. Tunapaswa kupambana pamoja dhidi ya vikwazo na magumu, bega kwa bega, kwa moyo mmoja.

Kama Wakristo wangetenda kazi kwa pamoja, wakisonga mbele kwa umoja, chini ya uongozi wa Nguvu moja, kwa ukamilishaji wa lengo moja, wangeugusa ulimwengu. (*Christian Service,* uk. 75)

Hakuna kazi kubwa zaidi kuliko uinjilisti wa vitabu, kwani uinjilisti huo unahusisha utendaji kazi wa majukumu ya kimaadili. Wale wanaoingia katika kazi hii wanahitaji kuwa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu daima. Haitakiwi pawepo na kujitukuza. Tuna nini ambacho hatukukipokea kutoka kwa Kristo? Tunapaswa kupenda kama ndugu, kudhihirisha upendo wetu kwa kusaidiana. Tunapaswa kuwa na huruma na heshima. Tunapaswa kupambana pamoja, tukienda sambamba. Wale tu wanaoishi ombi la Kristo, wakilifanyia kazi katika maisha halisi, watashinda jaribu linaloujia ulimwengu. Wale wanaojitukuza wanajiweka katika nguvu za shetani, wakijiandaa kupokea uongo wake. Neno la Bwana kwa watu wake ni kwamba tuinue viwango juu na juu zaidi. Kama tukitii sauti, atafanya kazi pamoja nasi, na juhudi zetu zitatunukiwa mafanikio. Katika kazi yetu tutapokea Baraka nyingi kutoka juu na tutaweka hazina pembeni ya kiti cha enzi cha Mungu. (*The Colporteur Evangelist,* uk. 25)

"Ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, mkinia mamoja. Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno, bali kwa unyenyekevu, kia mtu na mahesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake." (Wafilipi 2:2, 3)

Kuna roho ya kujitegemea kwa wingi iliyojikita kati ya wajumbe. Hii inapaswa kuwekwa kando, na na kazi ya Mungu ifanyike kwa pamoja kwa watumishi wake. Kumekuwa na roho ya kuuliza kwa wingi kusema, "Kwani mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" Alisema malaika, "Ndiyo, wewe ni mlinzi wa ndugu yako. Unapaswa kuwa mwangalizi wa ndugu yako, uwe na shauku kwa maendeleo yake, na kukuza roho njema yenye upendo kwake. Songeni mbele pamoja, songeni mbele pamoja," Mungu alidhamiria kwamba mwanadamu awe na moyo mweupe na mkweli, bila tabia ya kujifanya, mpole, mnyenyekevu, na mwepesi. Hii ni kanuni ya mbinguni; Mungu aliiagiza hivyo. (*Gospel Workers* [1892], uk. 259)

Kuna ubaridi na utofauti mkubwa sana – roho iliyopo kwa wingi ni ya "Sijali" – na inatenda kazi kati ya wafuasi wa Kristo. Wote wanapaswa kuhisi hali ya kujali wenzake, kujali ustawi wa wengine na kulea roho ya upendo kwao. "Pendanpeni." Ndipo tutakaposimama kama ukuta ulio imara dhidi ya mbinu za Shetani. Katikati ya upinzani na mateso hatutajiunga na wale wasiosamehe, hatutaungana na wafuasi wa mwasi mkuu, ambao kazi yao ya pekee ni kuwashtaki ndugu, kukashfu na kuchafua tabia zao.

Hebu masalia wa mwaka huu waboreshe katika kuharibu kila mzizi wa uchungu, na kuuzika katika kaburi pamoja na mwaka uliopita. Anza mwaka mpya na heshima, na upendo wa kina, kwa kila mshiriki wa familia ya Bwana. Songeni mbele pamoja. "Kwa umoja, tunasimama; kwa kutengana, tunaanguka." Chukua nafasi ya juu na yenye heshima zaidi kuliko ulivyofanya hapo kabla. (*Our High Calling,* uk. 370)

Ikiwa Shetani atachochea ukosoaji kati ya watu wa Bwana waliochaguliwa, utasambaa kama mwali wa moto kutoka kwa mmoja kwenda kwa mwingine. Usiipatie roho ya ukosoaji nafasi, kwani ni sayansi ya Shetani. Ukiikubali sayansi hii, ukaionea shauku, wivu, na dhana ovu za kuhisi hisi zinajitokeza.

Sogeleaneni kwa pamoja, ni agizo ninalolisikia kutoka kwa Nahodha wa wokovu wetu. Sogeleaneni kwa pamoja. Panapokuwa na umoja, pana nguvu. Wote walio katika upande wa Bwana watasonga mbele kwa pamoja. Kuna hitaji la umoja na upendo thabiti kati ya wale wanaoamini katika kweli, na chochote kinachopelekea mafarakano ni cha mwovu. Mungu amekusudia kwamba watu wake wawe na umoja na yeye kwa namna matawi yalivyo na umoja na mzabibu. Kisha watakuwa na umoja wao kwa wao. (*Selected Messages,* kitabu cha 3, aya. 351, 352)

Hebu kila mmoja atafute kujibu ombi la Kristo: “Kwamba wawe na umoja, kama wewe, Baba, Ulivyo ndani yangu, name ndani yako.” Ni umoja wa aina gani huu! Na Kristo anasema: “Hivyo wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.” (*Testimonies for the Church,* vol 5, aya. 488, 489)

SIKU YA NANE:

# URIMU NA THUMIMU

**Fungu elekezi: Waefeso 5:15-17**
"Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; mkiukomboa wakati maana zamani hizi ni za uovu. Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahaamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana."

**MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA**

**Kusifu**

- Bwana tunaanza kwa kukusifu kwa jinsi ulivyo – Kiongozi na Rafiki yetu.
- Tunakushukuru kwamba Biblia inaweka wazi mapenzi yako kwetu.
- Tunakusifu kwa kumtuma yesu, aliyekuja kudhihirisha mapenzi yako kwetu.

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama faragha. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhambi zetu.
- Utusamehe kwa nyakati ambazo hatukuwa tayari kufuata mapenzi yako yaliyoandikwa katika Neno lako.
- Tunakushukuru kwamba unatusamehe kulingana na 1 Yohana 1:9.

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Baba, tafadhali tusaidie kukumbuka kwamba mawazo yako kwetu ni mawazo "ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho" (Yeremia 29:11)
- Tunaomba kwa ajili ya mioyo inayofurahia kufanya mapenzi Yako, na si mapenzi yetu.
- Hebu kila mmoja wetu afuate mfano wa Yesu, aliyekuja sio afanye mapenzi yake bali afanye mapenzi ya Baba yake (Yohana 6:38)
- Bwana, tupatie hekima tunapotafuta mapenzi yako katika nyakati Fulani. Hebu na tukutafute na kutii Neno lako.
- Tunaombea vijana waelewe mapenzi yako kulingana na uchaguzi wa mwenzi wa maisha.
- Tafadhali waongoze na kuwaonyesha mapenzi yako wale uliowachagua kama viongozi wa kanisa.

- Tunaomba uwezeshe kusambazwa kwa miongozo ya Biblia, majarida, na vitabu kama "Jipatie Amani Moyoni". Hebu haya machapisho na yapande mbegu ya ukweli ndani ya mioyo ya watu na kuwaongoza kujifunza Neno la Mungu.
- Tunaomba uwawezeshe washiriki, wachungaji, na viongozi wengine duniani kote kujilisha katika Neno lako kila siku. Sisi pia utuwezeshe kukutafuta kila siku katika maombi binafsi. Utukumbushe kwamba hatuwezi kufanya jambo lolote bila wewe
- Tunakuomba Bwana utufanye kuwa tayari kukufuata katika nyanja za maisha yetu yote. Tunapotaka kupiga hatua inayofuata ya utii, utuoneshe ni ipi. Jaza maisha yetu kwa uwezo wako.
- Tunakuomba uhuishe mahudhurio ya Shule yetu ya Sabato duniani kote. Waongoze washiriki wote pamoja na wageni kupitia uzoefu wa uhusiano utokanao na badiliko la maisha, utume, kujifunza Biblia na kutoka na kuwaendea watu kama kanisa.
- Bwana, tunaomba kwa ajili ya watu saba (au zaidi) walio katika orodha binafsi za maombi. Hebu Roho Mtakatifu adhihirishe mapenzi yako ya kufundisha mmojawapo.
- Pia tunaomba kwa ajili ya mahitaji binafsi ya wale waliokusanyika hapa.

**Shukrani**

- Bwana, tunakushukuru kwamba upo tayari kudhihirisha mapenzi yako kwetu.
- Tunakushukuru kwamba tunapokuamini kwa mioyo yetu yote bila kutegemea akili zetu wenyewe, na tunapokukubali katika njia zetu zote, utaongoza njia zetu (Mithali 3:5, 6).

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Yote Namtolea Yesu (122); Twae Wangu Uzima (146); Uniongoze Jehova (156); Bwana Ninataka Hili (116); Yesu Furaha ya Moyo (23).

## URIMU NA THUMIMU

"Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; mkiukomboa wakati maana zamani hizi ni za uovu. Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahaamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana." (Waefeso 5:15-17)

**Upande wa kulia na wa kushoto wa kifuko cha kifuani kulikuwa na mawe mawili yaliyokuwa na mng'ao mkubwa. Haya yalijulikana kama Urimu na Thumimu. Haya mawe yalimsaidia kuhani kutambua mapenzi ya Mungu. Swali lilipoletwa mbele za Mungu ili aamue, udhihirisho wa ukubali ulionekana kwa kung'aa jiwe la upande wa kulia. La, kama Mungu hakuridhia, ukungu wenye weusi ulizunguka jiwe la upande wa kushoto. Ni muhimu kwetu kuelewa kazi ya Kristo kwa niaba yetu na mapenzi Yake kwa maisha yetu leo.**

Kila mtu ana nafsi ya kuokoa au kupoteza. Kila mmoja ana kesi inayosubiri kusikilizwa na Mungu. Kila mmoja anapswa kukutana na Hakimu mkuu uso kwa uso. Hivyo, ni muhimu kiasi gani, kwamba kila akili itafakari mara kwa mara tukio hili linalohusu wakati hukumu itakapowekwa na vitabu vitakapofunuliwa, wakati kila mtu anapaswa kusimama pamoja na Danieli, katika sehemu yake, katika mwisho wa siku. (*Evangelism,* uk. 222)

Katika mambo madogo na makubwa ya maisha swali la kwanza linapaswa kuwa, "Mapenzi ya Mungu ni yapi?" Kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia kuliko mafuta ya beberu." Kristo anawaita watoto wake kuachana na ubinafsi wa kila aina, tamaa zote, uchafu wote. "Njooni kwangu," Anasema, "nami nitawapumzisha." Jikiteni katika mafundisho yangu. Salimisheni mapenzi yenu kwa mapenzi yangu, njia zenu kwa njia zangu. Ruhusu maisha yenu yawe mamoja na maisha yangu. Hivyo mtapata thawabu ambayo itadumu hata uzima wa milele. (*Signs of the Times,* Feb. 19, 1902. aya. 13)

Mapenzi ya Mungu ni yapi? Nifanye nini ili nimtukuze Mungu? Ninawiwa kumtumikia Mwokozi wangu kwa moyo wote. Nikiyahesabu mambo yote kuwa kama mavi ili nipate Kristo. Mbingu, uzima wa milele, una thamani kuliko kila kitu kwangu, na Kristo alikufa ili niweze kumiliki utukufu ulio mzito wa milele… (*That I May Know Him,* uk. 203)

Kila jitihada inayofanywa kuvunja nguvu za tabia mbaya ni jitihada za kibinadamu. Ni mapenzi ya Mungu kwamba, kwa jitihada thabiti, tuinuke katika heshima ya usafi wa maisha, tukipata nguvu za kiroho, na kupata nguvu za kimaadili kupitia mazoezi ya vitengo Mungu alivyotupatia. Kuna furaha katika uwepo wa malaika wa mbinguni wakati vijana wanapopata ushindi katika jina la Yesu. (*The Youth Instructor,* Nov 12, 1896. aya. 6)

"Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu," aliandika mtume Paulo, "kutakaswa kwenu." 1 Thesalonike 4:3. Utakaso wa kanisa ni kusudi la Mungu katika mambo yake yote

anayofanya kwa wanadamu. Amewachagua tangu milele, kwamba wawe watakatifu. Akamtoa mwanawe ili kufa kwa ajili yao, ili waweze kutakaswa kupitia katika kutii ukweli, kuvuliwa ubinafsi wa kila aina. Kutoka kwao anahitaji jitihada binafsi na kujisalimisha kikamilifu. Mungu anaweza kuheshimiwa na wale wanaotangaza kumwamini, kadri wanavyohakikishwa katika sura yake na kuongozwa na Roho wake. Kisha, kama mashahidi wa Mwokozi, wanaweza kutangaza kile neema ya kimbingu ilichowatendea. (*The Acts of the Apostle,* uk 559)

"Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu," aliandika mtume Paulo, "kutakaswa kwenu." 1 Thesalonike 4:3. Je, ni mapenzi yako pia? Dhambi zako zinaweza kuwa kama milima mbele yako; lakini kama ukinyenyekeza moyo wako na kuungama, ukiamini faida ya Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka, atakusamehe na kukusafisha na udhalimu wote. Mungu anahitaji utii wako kamili wa sheria yake. Sheria hii ni mwangwi wa sauti yake ikikwambia, takatifu zaidi, ndio, takatifu zaidi. Tamani ujazo wa neema ya Kristo. Ruhusu moyo wako kujazwa na shauku kubwa ya haki yake, kazi ambayo Neno la Mungu hutangaza kwamba ni amani, na matokeo yake ni ukimya na uhakikisho wa milele. (*Acts of Apostles,* uk. 566)

Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya. (2 Wakorintho 5:17)

Fursa kubwa imetolewa ili watu wa Mungu wapate ukamilifu wa tabia. Mtume anasema, "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu." Hebu kila mmoja ajichotee kutoka katika chanzo kisichokoma cha nguvu za maadili na akili, ili kwamba aweze kufanya kazi za haki. Kupitia msalaba wa Kalvari kila kitu kimetengenezwa ambapo mwanadamu anaweaza kuwa na umoja na wanadamu wenzake, pia umoja na Kristo ndani ya Mungu. Baba anasema kwamba atawapenda wale wanaoamini kwamba Kristo aliwafia, kama anavyompenda Mwanawe pekee. Msalaba wa Kristo ni uthibitisho kwamba tunaweza kukamilika katika yeye. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Katika Kristo kuna uzuri, katika yeye kuna akili nyingi na maadili ya kutosha. (*Review and Herald,* Nov 30, 1897, aya 9)

Mungu anakunyooshea mkono mmoja, imani itashikilia mkono wake wenye nguvu, na kwa mkono mwingine, upendo uzifikie roho zinazopotea. Kristo ndiye njia, kweli, na uzima. Mfuate yeye, usitembee katika mwili, bali katika Roho. Tembea kama alivyotembea. Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu. Kazi

unayotakiwa kuifanya ni kuyatenda mapenzi yake yeye anayehudumia maisha yako kwa utukufu wake. Mkifanya kazi kwa ajili yenu wenyewe, haitawafaidia kitu. Kufanya kazi kwa mafanikio ya wengine, kutojijali sana na zaidi katika udhati kujitoa kikamilifu kwa Mungu, kutakubalika mbele yake na atawalipa kwa neema yake yenye utajiri. (*Testimonies for the Church,* vol. 2, uk. 170)

SIKU YA TISA:

## CHETEZO

**Fungu elekezi:** Waebrania 7:25

“Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee.”

**MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA**

**Kusifu**

- Bwana wetu, tunakusifu kwamba Yesu ni mwombezi wetu.
- Ahsante kwamba kadiri tunavyokusogelea kupitia kwa wema wa Kristo, tunafunikwa na vazi lake la kikuhani.

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Baba, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama faragha. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhambi hizo.
- Tusamehe hasa nyakati ambazo tumeshindwa kutambua upatanishi wa Yesu. Tuanomba utufundishe neema yake.
- Ahsante sana kwa kuwa unatusamehe kulingana na 1 Yohana 1:9

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Bwana, tusaidie kuelewa na kuthamini maombezi ambayo Yesu anafanya kwa ajili yetu.
- Tuoneshe mizigo ya wengine tunayotakiwa kuombea. Mwoneshe kila mmoja wetu ni nani wa kuombea.
- Tunawaombea wazazi ambao wanaofanya maombezi kwa ajili ya watoto wao ambao hawakupendi. Tunaomba kwamba uwawezeshe kuendelea kuomba wala wasiache.
- Tunawaombea wale ambao wamekata tamaa. Wawezeshe kujifunza kupeleka mizigo yao kwa Yesu.
- Bwana, tunawaombea watu ambao wamekoma kuja kanisani. Tusaidie kuwakaribisha kwa upendo wako pale wanapoamua kurudi.
- Tunakuomba uimarishe huduma ya kutoka na kuifikia jamii kwa kila kanisa mahalia. Huduma kama vile huduma za wanawake, Pathfinder, Adventurers, na

huduma ya Waadventista kwa jamii. Tuoneshe jinsi ya kuwa "mkono wako na miguu yako" kwa wengine.

- Bwana, tunakuomba uwezeshe uwepo wa uamsho ule wa kale katika kanisa lako katika siku za mwisho. Tuwezeshe kusimamia ukweli hata kama mbingu zingeanguka.
- Wabariki mashuhuda wa huduma ya mitandao ya Waadventista wa Sabato pamoja na mitandao ya kijamii. Wasaidie kuhakikisha wanakuwa bora kadiri tunavyowakaribia watu wa karne ya ishirini na moja tukiwa na injili ya milele.
- Bwana tupatie hisia za kustaajabu na kushukuru kadiri tunavyotafakari ulimwengu uliouumba. Tunaomba utuwezeshe kuuheshimu ukweli wa Biblia unaohusu uumbaji na kufundisha vijana wadogo kutambua uwezo wako na upendo wako katika uumbaji wako wa asili.
- Bwana, tufundishe kufuata mfano na kielelezo cha Yesu Kristo ambaye hakuwa na ubinafsi kabisa kwa kukabiliana kila siku na mahitaji ya watu walio karibu na sisi. Tuwezeshe kutumika kama wamisionari matabibu, wanaojitolea katika jamii, na rafiki wa wenye shida.
- Bwana, tunawaombea wale watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Wawezeshe kufungua mioyo yao kwa Roho Mtakatifu.
- Tunaomba pia kwa ajili ya mahitaji binafsi ya wale wote waliokusanyika hapa.

**Shukrani**

- Bwana, tunakshukuru kwa kuwa Kristo anafanya maombezi kwa ajili yetu, hivyo tuna tumaini na kutazamia mambo yajayo.
- Ahsante kwa kuwa "Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa." (Warumi 8:26)
- Tunakushukuru kwa kuwa Yesu, "aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee." (Waebrania 7:25)

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Nataka Nimjue Yesu (54); Nena Rohoni Yesu (15); Kuwa wake Yesu (149); Nitaonana na Yesu (175); Yesu kwa Imani (123)

## CHETEZO

Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee. (Waebrania 7:25)

**Chetezo na uvumba ni ishara ya maombezi ya Kristo kwa ajili yetu.**

Kama mwombezi wetu, anatimiza kazi yake aliyojipa mwenyewe, akishikilia chetezo chenye maombi ya thamani ya mitume wake mbele ya Mungu yakichanganyika na maungamo, na shukrani za watu wake. (*Christ Object Lessons*, uk. 156).

Kristo kama mpatanishi wetu, akiwa mkono wa kuume wa Baba, siku zote anatuona. Ni muhimu kwamba atuombee kwa vile alitukomboa kwa damu yake. (*Our High Calling,* uk. 50).

Ninashukuru kwa sababu tunaweza kumwamini Mungu, naye anaheshimiwa tunapomwamini, tukimpelekea mashaka yetu. Bwana ambaye ni Yehova hakuona kuwa kanuni ya ukombozi ilikamilika kwa kuwekeza kwenye upendo wake. Kwa uteuzi wake mwenyewe ameweka katika madhabahu yake wakili aliyevikwa hali ya asili. Kama mwombezi wetu, kazi yake kubwa ni kututambulisha kwa Mungu kama wana wake na binti zake. Kristo anafanya maombezi kwa niaba ya wale waliompokea. Hao anawapa uwezo, kwa faida yake mwenyewe anawafanya ni sehemu ya familia ya kifalme, wazao wa mfalme wa mbinguni. Na Baba anadhihirisha upendo wake usio na kikomo kwa Kristo ambaye alilipa gharama ya ukombozi kwa damu yake na hivyo kuwapokea na kuwakaribisha marafiki wa Kristo kama marafiki wake. Ameridhika na upatanisho uliofanyika. Ametukuzwa kwa kuzaliwa kwa Mwana wake, kuishi na kufa na hatimaye kufanya upatanisho.

Ni kujishusha kwa namna gani huko? Ni fursa kubwa kiasi gani hiyo tuliyopewa? Kristo ndiye kiungo kati ya Mungu na mwanadamu. Kadiri tunavyomsogelea Mungu kupitia kwa mema ya Kristo, tunavikwa joho lake la kikuhani. Anatusogeza pembeni yake, akitukumbatia kwa mkono wa kibinadamu na mwingine ukishikilia kiti cha enzi cha milele. Anafanya kustahili kwake kuwe kama uvumba mzuri ndani ya chetezo kilichopo mikononi mwetu ili kuhimiza kusihi kwetu. Anaahidi kusikia na kujibu maombi yetu. Naam, Kristo amekuwa ni mapito ya maombi kati ya mwanadamu na Mungu. Yeye pia amekuwa ni mapito ya mibaraka kati ya mwanadamu na Mungu. Ameunganisha uungu na ubinadamu. (*In Heavenly Places,* uk. 77)

Na kadiri Kristo anavyotuombea, Roho wa Mungu anafanya kazi ndani ya mioyo yetu, akiweka ndani yetu sala na toba, sifa na shukrani. Shukrani inayobubujika kutoka katika midomo ya mwanadamu ni matokeo ya mguso wa Roho, akigusa nyuzi za roho na kuamsha muziki mtakatifu.

Maombi, sifa na toba ya watu wa Mungu inapanda kama kafara hadi hekalu la mbinguni. Kupanda huku hakufanyiki katika usafi usio na doa, bali hupitia kwenye mifereji ya kibinadamu iliyoharibiwa na dhambi kiasi kwamba isingekuwa kutakaswa na haki ya Kuhani wetu Mkuu, haya maombi, sifa na toba visingekubaliwa na Mungu. Kristo anakusanya maombi, sifa na kafara za watu wake na kuziweka katika chetezo, pamoja na hivyo anachanganya na kustahili kwa haki yake isiyokuwa na doa. Kisha kwa manukato ya uvumba wa upatanisho wa Kristo, maombi yetu yanakamilishwa na kupaa mbele za Mungu. Ndipo majibu ya utukufu yanarudi. (*The Youth's Instructor*, April 16, 1903, aya ya 11, 12)

Uteuzi wa Mungu na vipaji vyake kwa niaba yetu havina kikomo. Kile kiti cha enzi chenyewe ni kivutio cha hali ya juu kwa sababu kinakaliwa na Yeye ambaye anaturuhusu tumwite Baba. Lakini Mungu hakuona kama kanuni ya ukombozi ilikuwa imekamilika akiwa amewekeza tu katika upendo wake. Kwa uteuzi wake mwenyewe aliweka katika madhabahu yake wakili aliyevikwa hali ya asili. (*Testimonies for the Church,* vol. 6, uk. 363)

"Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." (Waebrania 4:15, 16)

Pale mwanadamu anapoelekea kwenye kiti cha rehema ndipo anapokuwa mteja wa Wakili Mkuu. Anapoanza tu kutamka toba yake na kuomba msamaha, Kristo anamkubali na kupokea kesi hiyo na kuifanya ni ya kwake. Ndipo anapoiwakilisha kwa kusihi mbele ya Baba kana kwamba ni ya kwake yeye mwenyewe.

Kadiri Kristo anavyoendelea na maombezi kwa niaba yetu, Baba anafungua hazina zote za Neema yake kwa ajili yetu. Ili tuzifurahie na kuziwakilisha kwa wengine. Yesu anasema, "Ombeni kwa jina langu" na kuongezea kwamba, "Sisemi kwamba nitawaombea kwa Baba, kwani Baba mwenyewe anawapenda kwa sababu mmenipenda. Tumieni jina langu, litayapatia maombi yenu ubora wa pekee, na Baba yangu atawapeni utajiri wa neema. Hivyo "ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu." Yohana 16:24. (*Testimonies for the Church*, vol. 6, uk. 364).

SIKU YA KUMI:

## NJUGA NA MAKOMAMANGA

**Fungu elekezi: Luka 21:28**
"Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia."

**MPANGILIO WA MUDA WA MAOMBI UNAOPENDEKEZWA**

**Kusifu**

- Bwana tunakusifu kwa ajili ya kile ulichodhihirisha kwetu kama ishara ya kuja kwako mara ya pili.
- Tunakusifu kwa sababu Yesu anakuja tena kutuchukua ili tuwe pamoja naye milele.

**Kuungama na kudai ushindi dhidi ya dhambi**

- Bwana, tafadhali tuoneshe dhambi tunazotakiwa kuungama hadharani na zipi tunazotakiwa kuungama faragha. Tunadai ushindi wako dhidi ya dhambi zetu.
- Utusamehe tunaposhindwa kutambua ishara za kuja kwako mara ya pili kwa sababu ya kuridhika na kudhani tuna starehe hapa duniani.
- Ahsante kwa sababu unatusamehe kulingana na 1 Yohana 1:9

**Kujitoa na Kufanya Maombezi**

- Bwana, tunawaombea watu wanaotuzunguka ambao bado hawajatambua kwamba unakuja hivi karibuni. Tafadhali amsha mioyo yao
- Tafadhali tuoneshe vitu ambavyo hatujasalimisha katika maisha yetu. Tunakupatia vitu hivyo na kukuomba ubadilishe mioyo yetu.
- Tafadhali endelea kuumba upya tabia zetu na kututayarisha kwa ajili ya kuja kwako mara ya pili.
- Bwana, wasogelee watu ambao wanaogopa tukio la kuja kwako mara ya pili. Wafanye watoe maisha yao kwako.
- Tunaomba ututumie kila mmoja wetu kuwaambia wengine habari njema za ujio wako.
- Tuoneshe jinsi ya kushughulikia mahitaji ya wakimbizi ya kimwili na ya kiroho. Hebu kanisa letu lifahamike kwa upendo uliopo kwa watu wote bila kujali ni kina nani, au wanatoka wapi.

- Tunaomba kwa namna ya pekee kwa ajili ya wakimbizi futoka katika nchi ambazo zimefungiwa injili isitangazwe. Kadiri tunavyowatimizia mahitaji yao basi waongozwe kukufahamu wewe zaidi. Tunaomba ufungue milango kwamba waweze kurudi nchini kwao na kushiriki na wengine upendo wa Mungu
- Baba, tafadhali tupatie hisia za juu za kuelewa umuhimu wa kazi tunayofanya kwa ajili yako. Tuwezeshe kuishi tukiwa na tumaini kila siku kwamba Yesu anakuja hivi karibuni kufanya mambo yote kuwa mapya.
- Bwana tunakuomba ubariki kazi ya Waadventista wa Sabato wanaofundisha katika ngazi zote duniani kote. Waimarishe waalimu mashuleni, wazazi, viongozi wa vijana, na waalimu wa Shule ya Sabato kadiri wanavyotayarisha kizazi hiki cha vijana kwa ajili ya kukutumikia.
- Tunakuomba ubariki kazi ya huduma ya pekee kwa wahitaji. Tupatie mioyo ya huruma kadiri tunavyoshughulikia mahitaji ya vipofu, viziwi na wale ambao wana changamoto za kimwili au kiakili
- Bwana, tunawaombea wale watu saba (au zaidi) katika orodha zetu binafsi. Tunaomba uwawezeshe kutambua mahitaji yao na kutoa mioyo yao kwa Roho Mtakatifu ili afanye kazi katika maisha yao
- Tunaomba pia kwa ajili ya mahitaji binafsi ya wale wote waliokusanyika hapa.

Shukrani

- Bwana, ahsante sana kwa ahadi yako kwamba, "… yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu." Wafilipi 1:6
- Tunakushukuru kwamba unao watu katika kila mji wanaotazamia mbingu mpya.
- Ahsante sana kwa sababu unafanya kazi ndani ya mioyo ya wale watu tunaowaombea.

**Nyimbo za kuimba zinazopendekezwa**

Furaha kwa Ulimwengu (166); Mfalme yu Mlangoni (157); Ukingoni mwa Yordani (178); Kuwa na Yesu Nyumbani (204); Hapo Yesu Atakapoita (169)

## NJUGA NA MAKOMAMANGA

"Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia." Luka 21:28

**Njuga katika kanzu ya Kuhani Mkuu iliwapatia watu waliokuwa nje ishara inayosikika kwamba alikuwa hai na anaendelea kufanya maombezi kwa ajili yao katika mahali patakatifu pa patakatifu. Kadiri Kristo anavyoendelea na maombezi katika chumba cha Patakatifu pa patakatifu, hata kama hatuwezi kusikia njuga hizo katika joho lake, tunatakiwa kuwa makini kwa ishara ambazo zinaashiria kumalizika kwa kazi yake kama Kuhani Mkuu na kisha aje kama Hakimu na Mfalme**

Kuhani mkuu aliingia katika chumba cha pili (patakatifu pa patakatifu) mara moja baada ya matayarisho makubwa. Hakuna jicho la mtu mwingine lililoruhusiwa kuchungulia ndani ya kile chumba na kuona utukufu mkuu uliokuwa pale ila la kuhai mkuu peke yake. Hapo palikuwa ni mahali ambapo Mungu alichagua kudhihirisha utukufu wake. Kuhani mkuu aliingia mahali pale siku zote kwa kutetemeka. Watu waliokuwa nje walimsubiri kwa ukimya usiopimika wakifanya maungamo ya dhati. Tamaa yao kubwa ilikuwa ni kwamba Mungu awasamehe dhambi zao na kuwabariki. Mungu aliwasiliana na Kuhani Mkuu kutoka kwenye kile kiti cha rehema. Alipokawia kwa muda ndani ya hicho chumba, hofu iliwaingia watu wakidhani kuwa labda ni kwa ajili ya dhambi zao, au pengine ni za kuhani mkuu ndiyo maana utukufu wa Mungu umemwangamiza. Lakini pale sauti ya njuga zilizokuwa zimefungwa kwenye joho lake ziliposikika, walikuwa na amani wakijua kwamba yu hai humo. Ndipo hatimaye alitoka nje na kuwabariki watu. (*The Spirit of Prophecy*, vol. 1, uk. 274, 275)

Yesu alipokuwa akihudumu ndani ya chumba cha patakatifu pa patakatifu, nilisikia mlio wa njuga zilizokuwa zimening'inizwa kwenye joho lake, na alipotoka, wingu zito liliwafunika wakazi wa dunia hii. Wakati huo hapakuwa na mpatanishi kati ya mwanadamu mwenye hatia na Mungu aliyekosewa. (*Early Writings,* uk. 280)

Kristo aliwaagiza watu watu wake watazamie ishara za kuja kwake, na wafurahi kadiri zinavyoonekana kuashiria kuja kwa Mfalme. Aliwaambia kwamba, "Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia." Aliwaelekeza wafuasi wake kwenye mtini akisema, "…Utazameni mtini na miti mingine yote. Wakati iishapo kuchipuka, mwaona na kutambua wenyewe ya kwamba majira ya mavuno yamekwisha kuwa karibu. Nanyi kadhalika, mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu." (Luka 21:28-31) (*The Great Controversy*, [1888], uk. 308)

Pale kwenye mlima wa mizeituni Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuhusu tukio la kuja kwake mara ya pili hapa duniani. Alitaja ishara maalum zitakazoonesha kwamba

kuja kwake kumekaribia, na akawaagiza wakeshe na kuwa tayari. Alirudia maneno ya maonyo akisema, "Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa atakayokuja mwana wa Adam." Kisha akawaonesha maana ya kukesha kwa ajili ya kuja kwake. Muda hautakiwi kutumiwa kwa kukaa tu na kusubiri kizemba, bali kufurahia kufanya kazi yake. (*Christ Object Lesson,* uk. 325)

Wapo watu duniani leo hii ambao wanafumbia macho ushuhuda ambao Kristo aliutoa kutahadharisha watu kuhusu kuja kwake. Wanajaribu kuzima ule uwezo wa watu wa kuelewa, wakati hizo ishara alizotaja zikitimia kwa haraka sana na ulimwengu unajitayarisha kwa wakati huo ambao Mwana wa Adam atadhihirishwa katika mawingu ya mbinguni. Paulo anafundisha kwamba ni dhambi kujifanya haujui hizo ishara zinazoashiria kuja mara ya pili kwa Kristo. Yesu aliwaita wale walio na hatia ya uzembe huu kuwa ni wana wa usiku na wa giza. Anawahimiza wanaokesha kwa maneno haya: "Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi." (1 Thesalonike 5:4-6) (*The Acts of Apostles,* uk. 260)

Tunasumbuka sana kuhusu hali halisi ya sasa ya kanisa lenye washiriki ambao kwa muda mrefu wamekuwa na uelewa na elimu ya haya matukio yanayoendelea kutimia karibu na mwisho wa wakati katika kutimiza historia ya unabii. Yesu anakuja na uweza na utukufu mkuu, "na hao wafu watahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao." Yule aliyesimama kama mwombezi wetu, anayesikia maombi yote ya toba na maungamo, anayewakilishwa na upinde wa mvua ambayo ni ishara ya neema na upendo, ukiwa umezunguka juu ya kichwa chake, hivi karibuni atakoma kufanya kazi anayofanya katika hekalu la mbinguni. Ndipo neema na rehema vitashuka kutoka katika kiti cha enzi, na haki itachukua nafasi. Yeye ambaye watu wake wamekuwa wakimwangalia, atashika nafasi yake – yaani ofisi ya Hakimu Mkuu. "Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote… Naye akampa amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni Mwana wa Adamu." Petro anasema kuwa ni yeye aliyeagizwa kwamba, "Nao watatoa hesabu kwake yeye aliye tayari kuwahukumu walio hai na waliokufa." Amechagua siku atakayouhukumu ulimwengu kwa haki kwa yule mtu aliyemchagua na kumweka wakfu. (*Review and Herald*, Jan.1 1889, aya ya 1)

# AHADI ZA KUDAI KATIKA MAOMBI

**Ahadi za Roho Mtakatifu**

“Mwombeni Bwana mvua wakati wa masika, naam, Bwana afanyaye umeme, naye atawapa manyny ya mvua, kila mtu atapewa nyasi kondeni.” Zakaria 10:1

“Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao.” Luka 11:13

“Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia… Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.” Yohana 14:26; 16:8

“Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.” Yohana 14:12-14

“Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi.” Zakaria 4:6

**Ahadi kwamba Mungu Hujibu Maombi**

“Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.” Yohana 15:7

“Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.” Waebrania 4:16

“Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Marko 11:24

“Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitukuza.” Zaburi 50:15

“Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni.” Mathayo 18:19

“Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea.” Mathayo 21:22

"Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana." Yohana 14:13, 14

"Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin, nawaambia, Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu."Yohana 16:23, 24

"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia." 1 Yohana 5:14, 15

**Ahadi Kuhusu Nguvu ya Mungu**

"Kuna neno gani lililo humu la kumshinda Bwana? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na sara atapata mwana wa kiume." Mwanzo 18:14

"Bwana atawapigania ninyi, nanyi mtanyamaza kimya." Kutoka 14:14

"Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yawezekana kwa Mungu." Marko 10:27

"Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya." 1 Thesalonike 5:24

"Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika." Ayubu 42:2

"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" Warumi 8:31, 32

"Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza?" Hesabu 23:19

"Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; akili zake hazichunguziki. Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo. Hata vijana watazimia na kuchoka, na wanaume vijana wataanguka; bali wao wamngojeao bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu wala hawatazimia." Isaya 40:28-31

**Ahadi kwa ajili ya Ulinzi wa Mungu**

"Je! Si mimi niliyekumuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako." Yoshua 1:9

"Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia." Mwanzo 28:15

"Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengenezea." Kutoka 23:20

"Lakini huko, kama mkimtafuta Bwana, Mungu wako, utampata, ukimtafuta kwa moyo wako wote, na roho yako yote." Torati 4:29

"Niite, nami nitakuitikia, nami nitakonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua." Yeremia 33:3

"Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa." Isaya 40:4, 5

"Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea; Nitakushauri, jicho langu likikutazama." Zaburi 32:8

"Naye Bwana, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike." Torati 31:8

"Ni nani amchaye Bwana? Atamfundisha katika njia anayoichagua." Zaburi 25:12

"Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe." Mithali 3:5, 6

"Na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri." Isaya 58:10, 11

"Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu; na wakiwa katika kunena, nitasikia." Isaya 65:24

**Ahadi kwa ajili ya Moyo Uliobadilishwa**

"Nami nitawapa moyo, wanijue ya kuwa mimi ni Bwana; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao; kwa maana watanirudia kwa moyo wao wote." Yeremia 24:7

"Bwana, Mungu wako, atautahiri moyo wako, na moyo wa uzao wako, ili umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, upate kuwa hai." Torati 30:6

"Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama." Ezekieli 36:26

"Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu." Wafilipi 1:6

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya." 2 Wakorintho 5:17

"Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2: 20

"Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu n miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo." 1 Wathesalonike 5:23, 24

**Ahadi kwa Msamaha**

"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." 2 Nyakati 7:14

"Kwa maana Wewe, Bwana, U mwema, Umekuwa tayari kusamehe, Na mwingi wa fadhili, Kwa watu wote wakuitao." Zaburi 86:5

"Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu." Marko 11:25

"Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi." Waefeso 4:32

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 19

"Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu." Isaya 1:18

"Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako." Isaya 43:25

"Maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena." Yeremia 32: 34

"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake." Waefeso 1:7

**Ahadi kwa Ushindi Dhidi ya Dhambi**

"Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu." 1 Yohana 5:4

"Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda." Warumi 8:37

"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." 1 Wakorintho 15:57

"Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu." Isaya 41:10

"Zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya Yule mwovu." Waefeso 6:16

"Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2: 20

"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Wafilipi 2:13

"Basi nasema, Enendeni kwa Roho, waa hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili." Wagalatia 5:16

"Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe pamoja nanyi. Amina." Warumi 16:20

"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu." Warumi 12:2

"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake." 1 Yohana 2:15

**Ahadi za Uponyaji**

"Akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzshika amri zake, mimi sitatia juu yako maadhi yo yote niliyowatia Wamisi; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Kutoka 15:26

"Makomeo yako yatakuwa ya chuma na shaba; Na kadiri ya siku zako ndivyo zitakavyokuwa nguvu zako." Torati 33:25

"Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, Wala usizisahau fadhili zake zote. Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote, Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema, Aushibisha mema uzee wako, Ujana wako ukarejezwa kama tai." Zaburi 103:2-5

"Usiwe mwenye hekima machoni pako; Mche Bwana, ukajiepushe na uovu." Mithali 3:7, 8

"Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona." Isaya 53:3-5

"Uniponye, Ee Bwana, name nitaponyeka; uniokoe, name nitaokoka; kwa maana wewe ndiwe uliye sifa zangu." Yeremia 17:14

"Maana nitkurudishia afya, nami nitakuponya jeraha zako, asema bwana, kwa sababu wamekuita, mwenye kutupwa, wakisema, Ni Sayuni, ambao hapana mtu autakaye." Yeremia 30:17

"Tazama, nitauletea afya na kupona, name nitawaponya; name nitawafunulia wingi wa amani na kweli." Yeremia 33:6

"Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langum jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini." Malaki 4:2

"Mtu kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana." Yakobo 5:14, 15

**Ahadi kwa ajili ya Nguvu za Kufanya Mapenzi ya Mungu**

"Umngoje Bwana, uwe hodari, Upige moyo konde, naam, umngoje Bwana." Zaburi 27:14

"Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku wa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele." 2 Wakorintho 4:16-18

"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho." Wagalatia 6:9

"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu." Wafilipi 4:13

"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Wafilipi 2:13

"Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza kwa Kristo ukae juu yangu." 2 Wakorintho 12:9

**Ahadi Kuhusu Kuwa Mashahidi wa Mungu**

"Msiogope wala msifanye hofu; je! Sikukuhubiri haya zamani na kuyaonyesha? Na ninyi ni mashahidi wangu. Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine." Isaya 44:8

"Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia." Isaya 60:1

“Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho.” 2 Wakorintho 5:18

“Lakini Bwana akaniambia, Usiseme, Mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru.” Yeremia 1:7

“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.” Matendo 1:8

“Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.” 1 Petro 2:9

“Mwe tayari siku zote kumjibu kila awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.”

## Kuhani Mkuu

Mavazi ya Kuhani Mkuu yalitengenezwa kwa aina ya vitambaa vilivyokuwa vya gharama sana, na yalitengenezwa kwa namna ya kupendeza kwa ufundi mkubwa sawasawa na daraja hilo lililokuwa la juu sana. Pamoja na vazi la kitani alilovaa kuhani, alikuwa na joho la rangi ya samawi juu yake, ambalo pia lilifumwa kuwa kipande kimoja. Kwenye upindo wake liliwekewa njuga za dhahabu na makomamanga ya rangi ya samawi, zambarau, na nyekundu. Upande wa nje kulikuwa na naivera, ambayo ilikuwa ni vazi fupi la rangi ya samawi, zambarau, nyekundu na nyeupe. Ilishikizwa na mkanda wenye mchanganyiko wa rangi hizo hizo ukitengenezwa kwa namna ya kupendeza. Naivera haikuwa na mikono, na katika mabega yaliyokuwa yametarizwa na nyuzi za dhahabu kulikuwa na vito viwili vya shohamu, vilivyokuwa na majina ya makabila kumi na mawili ya Israeli.

Juu ya naivera kulikuwa na kifuko cha kifuani, hiki kilikuwa ni kitakatifu sana katika mavazi ya kikuhani. Kilitengenezwa kwa namna naivera ilivyotengenezwa. Sura yake kifuko cha kifuani ilikuwa ni ya mraba upana wa naivera, kilining’inizwa kutoka mabegani kwa utepe wa samawi ulioshikizwa kwa pete za dhahabu. Upindo wa kifuko hiki uliwekewa vito kadhaa vya thamani sawa sawa na vito vinavyooneshwa kutengeneza misingi ya ule Mji wa Mungu. Pembeni kabisa kulikuwa na mawe kumi na mawili ya dhahabu yaliyopangwa kwa safu nne, na haya pia yalichongwa majina ya makabila ya Israeli. Agizo la Bwana lilikuwa ni kuwa, “Na Haruni atayachukua majina ya wana wa Israeli katika kile kifuko cha kifuani cha hukumu juu ya moyo wake, hapo atakapoingia ndani ya mahali patakatifu, kuwa ukumbusho mbele ya Bwana daima.” Kutoka 28:29. Kwa hiyo Kristo aliye Kuhani Mkuu, akimsihi Baba kwa ajili ya damu yake kwa niaba ya wenye dhambi, anayo majina katika moyo wake ya walioamini wakatubu na kuungama . Mtunga Zaburi anasema, “Nami ni maskini na mhitaji, Bwana atanitunza. Ndiwe msaada wangu na mwokozi wangu, Ee Mungu wangu, usikawie.” Zaburi 40:17

Upande wa kulia na wa kushoto wa kifuko cha kifuani kulikuwa na mawe mawili yaliyokuwa na mng’ao mkubwa. Haya yalijulikana kama Urimu na Thumimu. Haya mawe yalimsaidia kuhani kutambua mapenzi ya Mungu. Swali lilipoletwa mbele za Mungu ili aamue, udhihirisho wa ukubali ulionekana kwa kung’aa jiwe la upande wa kulia. La, kama Mungu hakuridhia, ukungu wenye weusi ulizunguka jiwe la upande wa kushoto.

Kofia ya kuhani mkuu ilikuwa ya kitani nyeupe ikiwa na upindo wa samawi, na utepe wa dhahabu wenye maneno haya: “Mtakatifu kwa Yehova.” Kila kitu kilichounganika na mavazi pamoja na mwenendo wa kuhani mkuu kilikusudiwa kuleta mguso kwa yeyote aliyemwona na kuhisi utukufu wa Mungu, utakatifu wa ibada yake, na usafi unaotakiwa kwa wale wanaosogelea uwepo wake. (*Partiarchs and Prophets*, uk. 350, 351).